**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| MHE. ZUBEIR ALI MAULID | - | SPIKA |
| 1. Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake |
| 2. Mhe. Shehe Hamad Mattar | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni |
| 3. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda |
| 4. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka |
| 5.Mhe. Haji Omar Kheri | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu |
| 6. Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi |
| 7. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 8. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge |

| | | |
|---|---|---|
| 9. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | - | MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 10. Mhe. Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake |
| 11. Mhe. Balozi Amina Salum Ali | - | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 12.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume | - | MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais |
| 13. Mhe. Rashid Ali Juma | - | MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani |
| 14. Mhe. Hamad Rashid Mohamed | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais |
| 15. Mhe. Maudline Cyrus Castico | - | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais |
| 16. Mhe. Salama Aboud Talib | - | MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake |
| 17. Mhe. Juma Ali Khatib | - | MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais |
| 18. Mhe. Said Soud Said | - | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais |

| | | |
|---|---|---|
| 19. Mhe. Khamis Juma Mwalim | - | Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe |
| 20. Mhe. Harusi Said Suleiman | - | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete |
| 21. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri | - | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani |
| 22. Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi |
| 23. Mhe. Chum Kombo Khamis | - | Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake |
| 24. Mhe. Lulu Msham Abdalla | - | Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake |
| 25. Mhe. Juma Makungu Juma | - | Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini |
| 26. Mhe. Abdalla Ali Kombo | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 27. Mhe.Abdalla Maulid Diwani | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 28. Mhe. Ali Khamis Bakar | - | Jimbo la Tumbe |
| 29. Mhe. Ali Salum Haji | - | Jimbo la Kwahani |
| 30. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) | - | Jimbo la Kijitoupele |
| 31. Mhe. Ame Haji Ali | - | Jimbo la Nungwi |
| 32. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - | Nafasi za Wanawake |
| 33. Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Kiwengwa |
| 34. Mhe. Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |

35. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
36. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
37. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
39. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
40. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
42. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
43. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
44. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
45. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
46. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
47. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
48. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
49. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
50. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
51. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
52. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
53. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
54. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
55. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
56. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
57. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
58. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Jimbo la Chukwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

| | | |
|---|---|---|
| 71. Mhe. Salma Mussa Bilal | - | Nafasi za Wanawake |
| 72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Nafasi za Wanawake |
| 73. Mhe. Shaib Said Ali | - | Jimbo la Chonga |
| 74. Mhe. Shamata Shaame Khamis | - | Jimbo la Micheweni |
| 75. Mhe. Simai Mohammed Said | - | Jimbo la Tunguu |
| 76. Mhe. Suleiman Makame Ali | - | Jimbo la Ziwani |
| 77. Mhe. Suleiman Sarahan Said | - | Jimbo la Chakechake |
| 78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi | - | Nafasi za Wanawake |
| 79. Mhe. Ussi Yahya Haji | - | Jimbo la Mkwajuni |
| 80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir | - | Nafasi za Wanawake |
| 82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 83. Mhe. Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |
| 84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar | - | Nafasi za Wanawake |

| | | |
|---|---|---|
| Ndugu Raya Issa Msellem | - | Katibu wa Baraza la Wawakilishi |

**Kikao cha Nne – Tarehe 25 Mei, 2016**

*(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)*

**Dua**

Mhe. Spika *(Mhe. Zubeir Ali Maulid)* Alisoma Dua

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2013/2014. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2013/2014 na Ripoti ya Ukaguzi yakinifu ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2013/2014, pamoja na Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) mwaka 2011/2015.

**Mhe. Rashid Makame Shamsi (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC)):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC), naomba kuweka hati mezani kuhusu Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC), kuhusiana na Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 2013/2014. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 2013/2014. Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2013/2014 na Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo CDF mwaka 2011/2015.

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 34

### Ucheleweshwaji wa Kesi Kupatiwa Hukumu

**Mhe. Salma Mussa Bilal (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) –** Aliuliza:-
Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kupewa majukumu ya kufungua kesi na kusimamia kazi ambayo ilikuwa ikifanywa na Jeshi la Polisi.

a) Kwa nini kumekuwepo na ucheleweshaji mkubwa wa kesi kusikilizwa kwa wakati kutokana na kutokamilika kwa ushahidi na wananchi kulazimika kushuka na kupanda katika majengo ya Mahakama.
b) Uamuzi wa Ofisi ya *DPP* kupewa kazi ya kufungua kesi ya kusimamia kumeleta tija gani kama kesi zinaendelea kuchelewa kutolewa hukumu kati ya miaka 2 na 5.
c) Ucheleweshaji wa kesi unazingatia vipi juu ya misingi ya Utawala Bora, wakati Serikali ya Awamu ya (7) inaendeleza mwelekeo wake wa kuimarisha Utawala Bora Zanzibar.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mara baada ya kesi kufunguliwa Mahakamani kinachotakiwa kwa upande wa Mkurugenzi wa Mashtaka ni kuwasilisha ushahidi, ili kuthibtisha kosa dhidi ya mtuhumiwa. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto mbali mbali ambazo zinasababisha ucheleweshaji wa kesi kusikilizwa Mahakamani. Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na:-

- Baadhi ya wananchi kutokuwa tayari kutoa ushahidi kwa sababu mbali mbali, ikiwemo muhali, au kuafikiana baina ya Mshtakiwa na Mlalamikaji na hatimae kuacha kuja kutoa ushahidi Mahakamani;
- Washtakiwa kutoroka dhamana na kusababisha kesi kukaa muda mrefu bila kusikilizwa;

- Uhamisho wa Mahakimu ambao unasababisha baadhi ya Washtakiwa kuomba kesi ianze kusikilizwa upya, kitu ambacho baadhi ya mashahidi hugoma kuja kutoa ushahidi wao kwa sababu wanahisi kusumbuliwa' na
- Dharura nyengine mbali mbali, ikiwemo dharura za Mawakili wa Washtakiwa kuitwa kwenye Mahakama nyengine za juu.

(b) Mhe. Spika, miongoni mwa tija zilizopatikana baada ya serikali kuanzisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni pamoja na:-

- Kuharakisha uendeshaji wa kesi za jinai na kupunguza mrundikano wa kesi hizo, kwani hivi sasa kesi haifunguliwi mpaka upelelezi wake ukamilike;
- Kuimarisha misingi ya Utawala Bora (*check and balance*) na uwajibikaji kwani, ili kesi ifunguliwe Mahakamani lazima ushahidi wake uzingatiwe na vyombo viwili (*DPP* na Polisi); na
- Kupunguza uwezekano wa wananchi kubambikiziwa kesi bila ya hatia.

(c) Mhe. Spika, moja ya misingi ya Utawala Bora ni kuhakikisha kwamba kunakua na Utawala wa Sheria miongoni mwa jamii. Hivyo, ni vyema wananchi wakaendelea kushirikiana na vyombo vyetu vya Sheria katika kutoa ushahidi, ili kuharakisha utoaji wa haki na kuimarisha Utawala Bora nchini.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kero za wananchi hivi sasa kuwa mahakama zetu zinachelewesha maamuzi yao au utaratibu wao katika kutoa hukumu ambapo huchukua muda mrefu. Lakini katika jibu Mhe. Waziri katuambia kwamba kuna changamoto kadhaa ambazo zinasababisha hivi.

Mhe. Spika, mimi nauliza hivi katika changamoto nyengine ambayo hakuitaja. Kwa kuwa wananchi wengi wanalalamika kwamba wanapoitwa kwenda kutoa ushahidi hawalipwi nauli ya kwenda na kurudi. Je, haoni hiyo ni changamoto kubwa ambayo wananchi wanavunjika moyo kwenda katika mahakama hizo?

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, ni kweli kabisa kwamba miongoni

mwa changamoto ambazo tunakabiliwa nazo ni pamoja na baadhi ya mashahidi wanapofika mahakamani kutokuwa na fedha za kuwalipa.

Mhe. Spika, lakini wizara yangu imekuwa ikijitahidi katika suala hili ili kuhakikisha kwamba changamoto hizi zinatoweka na husasani pale tunapokuwa na bajeti ya kutosha kufanya hivyo.

**Mhe. Mussa Foum Mussa:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba ucheleweshaji wa kesi ni kwa sababu ya kutohudhuria wale wanaotoa ushahidi. Lakini kuna baadhi ya kesi nyengine huwa mashahidi wameshakwenda mahakamani na mambo yote yamekamilika, lakini uwamuzi unachelewa.

Je, ni kwa sababu gani ule utoaji wa maamuzi unachelewa na mashahidi wameshatoa ushahidi wao?

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa kawaida baada ya ushahidi kukamilika na mahakama kukamilisha taratibu zake zote, kwa kawaida huwa haichelewi kutoa maamuzi yake.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kama lilivyo swali mama linasema, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kupewa majukumu ya kufungua kesi, wakati hapo mwanzo suala hili lilikuwa ndani ya mikono ya Polisi.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri, katika mwaka 2015/2016 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imefungua kesi ngapi na kati ya kesi hizo ngapi zimehukumiwa na kesi ngapi hazijapata kuhukumiwa, ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa kuwa swali la Mhe. Shadya Mohamed linahitaji takwimu, naomba kumwasilishia jawabu lake kwa njia ya maandishi. *(Makofi)*

**Nam. 84**

**Kutumiwa kwa Mashamba Yasiyotumika kwa ajili ya Kilimo**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said –** Aliuliza:-

Kwa kuwa Kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu na ardhi yetu ya Zanzibar imekua ikikubali mazao ya muda mfupi kama vile mpunga, muhogo na migomba. Kwa kuwa baadhi ya wananchi wamekuwa wakimiliki maeneo makubwa bila ya kuyatumia.

Kwa nini Serikali isiyatumie mashamba hayo kwa kuyalima mazao ya muda mfupi mpaka pale wamiliki wake watakapokuwa tayari kuyatumia.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 84 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mfumo wa Kilimo cha Konde ni maarufu hapa Zanzibar, wakulima wengi wamekuwa wanaazima maeneo ya kilimo kwa ajili ya kulima mazao ya muda mfupi ikiwemo viazi vitamu, matikiti na mboga. Mfumo huu umewasaidia wakulima wengi ambao hawamiliki ardhi. Hivyo tunaliomba Baraza lako, tuwe karibu sana na Mhe. Mwakilishi kuwajuwa hao wamiliki kwa lengo la kuhamasisha wamiliki na wakulima matumizi ya maeneo hayo.

Kwa vile serikali jukumu lake ni kushajihisha wakulima na sio kulima wenyewe. Ila sio busara ardhi ikiachwa haiendelezwi wakati wananchi wanahitaji kwa maendeleo yao. Kwa upande wa serikali tutafanya utafiti ili kuzibaini Konde hizo na hatimaye tukaye na wenye mali ili tufikie muafaka.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa serikali inawezekana ikawa vigumu kushuhulikia ulimaji kwenye mashamba hayo. Je, serikali haioni umuhimu wa kutoa tamko kwa wenye maeneo hayo kuyatumia wananchi wa kawaida kwa kushauriana na mmiliki wa eneo hilo na hata akikataa serikali ikalazimisha?

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Mwakilishi haya ni maeneo ambayo yanamilikiwa na wananchi na sio miliki ya serikali. Kwa hivyo, sisi kama tulivyosema kwamba tukishayabaini tutakaa nao na kuweza kuwahamasisha, ili kama wao wenyewe

binafsi hawawezi kulima, basi wawakodishe wananchi wengine ambao labda wanaweza kulima kwa kilimo cha muda mfupi.

**Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Tungependa kujua serikali inamiliki hekta ngapi za kilimo na watu binafsi wanamiliki hekta ngapi za kilimo ndani ya Zanzibar. Vile vile hawa watu binafsi katika hizi hekta ambazo wanamiliki ni wangapi, wanalima na katika hizi zinazomilikiwa na serikali ni ngapi zinatumika kwa ajili ya kilimo na ngapi zimekaa tu hazitumiki, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, kutokana na swali lake alilouliza anahitaji takwimu za hekta ngapi serikali inazo na hekta ngapi zinamilikiwa na watu binafsi, basi ningeomba kumjibu kwa maandishi. *(Makofi)*

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Welezo, napenda nichukuwe fursa hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, swali mama linazungumzia mashamba yanayoachwa na wananchi hayalimwi.

Lakini tukumbuke Mhe. Spika, nchi hii ni masikini watu wengi sana wanategemea kilimo, ili wapate chakula chao cha kila siku. Sasa wanayawacha mashamba haya kulima kwa sababu kwanza wezi wamezidi katika yale mashamba, wanalima hawapati kitu. Sababu ya pili serikali haiwasaidii vitu ambavyo vingeweza kuwasaidia wakaweza kupata yale mazao.

Je, wizara yako ina mkakati gani wa kuwasaidia wakulima wetu wadogo wadogo wanaolima haya mashamba kwanza waweze kupata haya mazao yao kujinusuru na wezi.

La pili kuwasaidia baadhi ya mambo, kwa mfano mbolea na utaalamu. Bajeti tutakuwa tunawapa mapesa mengi hapa lakini hatuoni faida kwa wale watu, mwisho kama alivyosema wanayawacha yale mashamba. Je, wizara yako ina mkakati gani?

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, mashamba ya watu binafsi, ni jukumu lao wao wenyewe kukaa wakalinda mazao yao, sio jukumu la serikali.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuwasaidia, tunaendelea kutoa taaluma jinsi gani ya kulima na jinsi gani ya kutumia mbolea pamoja na pembejeo. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante kwa majibu nampa Mhe. Waziri kwa majibu ya ziada.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ya maandishi na nyongeza, ila nataka niongezee tu hapa mwisho Mheshimiwa alitaka kujua Serikali inawasaidiaje wakulima hawa. Hii ni Serikali peke yake ambapo wakulima wanapewa asilimia 80% ya gharama za kuzalisha katika mbolea na pembejeo, hakuna Serikali nyengine duniani inayotoa asilimia 80% ya msaada kwa wakulima wake.

Cha kusikitisha Mhe. Spika, baadhi ya wakulima wanasaidiwa wanapewa pembejeo, lakini wanaziuza hawazitumii. Baadhi ya wakulima wanapewa taaluma hawaitumii taaluma ambayo wanapewa, kwa hivyo yapo mambo hapa mawili uko upande wa Serikali kutimiza wajibu wake, lakini upo upande wa wakulima wenyewe kutimiza wajibu wake.
Tutaendelea kuwaelimisha na tutaendelea kutoa huduma, lakini nasema mzigo mkubwa Serikali inabeba na nafikiri wakulima wange-*appreciate* juhudi za Serikali zinazofanywa katika sekta hiyo.

**Nam. 54**

**Kukwama kwa Matengenezo Uwanja wa Gombani**

**Mhe. Nassor Salim Ali** - Aliuliza:

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein katika moja ya ziara zake Kisiwani Pemba alifanya ziara katika Uwanja wa Gombani na kukagua vifaa mbali mbali vya ujenzi wa tatani kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya mchezo wa mbio za riadha. Kwa kuwa uwanja wa Gombani ulikuwa unategemewa kumaliza matengenezo hayo katika Sherehe za Mapinduzi za mwaka 2016 lakini mpaka leo bado.

a) Je, ni tatizo gani linalokwamisha kumaliza matengenezo ya uwanja huo.
b) Ni Kampuni gani inayotengeneza tatani za Uwanja huo na chini ya mtaalamu gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo** - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 lenye vipengele (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein alifanya ziara katika Uwanja wa Gombani na kukagua sehemu mbali mbali ikiwemo ujenzi wa tatani ya kukimbilia.

Mhe. Spika, ujenzi wa njia ya kukimbilia unakua hatua mbili. Hatua ya kwanza ni kujenga njia hiyo kwa lami ambayo inaitwa kitaalamu "*BASE"* na hatua ya pili ni uwekaji wa tatani juu ya njia ya lami.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, matatizo yaliokwamisha kumalizika kwa matengenezo ya uwanja huo ni kama ifutavyo:-

Kampuni ya *NOWES Investment* ambayo ilipewa kazi ya kuweka lami (kujenga *BASE*) ilicheleweshа kukamilisha kazi hiyo.

Kampuni hiyo ya *NOWES Investment* mbali na kucheleweshа kazi hiyo lakini pia kwenye maeneo ya magoli na sehemu ya *VIP* wanaposhukia viongozi walifanyakazi kwa kiwango cha chini sana ambapo italazimika ifanywe tena. Mbali na tatizo la hali ya hewa lakini imethibitishwa kuwa Kampuni hii haikufanya kazi zake kwa makubaliano.

(b) Mhe. Spika, Jina la Kampuni itakayotengeneza tatani ni *"**GUANGZHOU JRACE ATHLETIC FACILITIES COMPANY LIMITED**"* kutoka China na Wataalamu Elekezi *(Consultant)* ni *Samkay Consultant Company* ya Zanzibar.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Spika, pamoja na makjibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye kifungu a na b.

Mhe. Spika, kwanzan impongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini mbali na majibu hayo katika majibu yake nikiri kwamba kampuni hii ilicherewesha kukamilisha kazi ambayo ilipewa, kwa vile ilicherewesha.

a) Je, ni hasara gani Serikali imepata kwa kuchelewa kwa kazi hiyo.

b) Mhe. Spika, kwa kuwa kampuni hiyo haikufanya kazi zake kwa makubaliano ambayo walikubaliana na Serikali, je, ni hatua gani imechukua Serikali ili kudhibiti kampuni hiyo?

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, nakubaliana na Mheshimiwa kwamba kucherewesha au kuchelewa kwa ujenzi huu Serikali imeingia gharama, kwa hivyo nataka kumwambia Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali imebidi itafute baadhi ya vifaa vyengine kwa sababu vifaa vilivyonunuliwa kwa ajili ya kazi hii viliharibika, kwa hivyo hii ni hasara kwa Serikali.

La pili Mhe. Spika, hatua iliyochukua Serikali kupitia Wizara ya Habari Utamaduni, Utalii na Michezo kwanza ni kumsitisha huyu mkandarasi na kuondoa ubia wetu kati ya sisi na yeye na kutafuta mkarandasi mwengine ndugu yetu kutoka China na kujenga huu uwanja.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri hakujibu ni hasara ya kiasi gani ambayo Serikali imepata kutokana na uzembe ule ambao umefanya kampuni ile ya mwanzo, naomba kumuuliza tena Mhe. Waziri ni kiasi gani ambacho Serikali imepata hasara kutokana na kuchukua kampuni hii ya mwanzo ambayo ilitakiwa kujenga uwanja huu wa Gombani.

Vile vile ni vigezo gani Serikali inachukua kabla ya kuipatia kampuni tenda.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Nimuombe Mhe. Muwakilishi kwamba suala lake la Serikali limeingia hasara kiasi gani, kwa kuwa suala hili linahitaji majibu mazuri na ya takwimu na kwa faida ya Wawakilishi wengine, hili namuomba nimjibu kwa njia ya maandishi, kwa faida yetu wote na kwa jamii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba arejee suali lake la (b) sikulielewa.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Ni vigezo gani ambavyo Serikali inachukua kabla ya kuipa kampuni tenda ya kufanya chochote juu ya Serikali.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa majibu mazuri aliyoyatoa.

Mhe. Spika, naomba kuongezea tu na kujibu suala la pili la Mheshimiwa kama ifuatayo:

Mhe. Spika, pamoja na kwamba kuliulizwa suala la kitwakimu na likatakiwa takwimu halisi kama ilivyoelezwa, tutaleta kwa maandishi kama alivyoahidi Mhe. Naibu Waziri, lakini ieleweke kwamba asilimia ishirini ya malipo ambayo alitakiwa kukamilishiwa mkandarasi yule hayakulipwa yamesitishwa, kwa hivyo hasara iliyoingia pale ni asilimi 80% ambayo asilimia 40% alitanguliziwa wakati wa kazi na asilimia 40% huwa anapaswa kupewa pale anapoendelea na kazi. Na baada ya kubainika tu kazi haina kiwango mkataba ndipo ulipositishwa.

Mhe. Spika, suala la pili ni kwamba hatua gani zinazochukuliwa na vigezo gani vinavyotumiwa kuweza kumpata mkandarasi kupitia tenda zile, wakati kazi inapoanzishwa tenda hutolewa na tenda huwa ina vigezo vyote.

Kwa mujibu wa majibu ya tenda yanayowasilishwa na yule ambae ana-*qualifiy* (anakidhi vigezo) vya tenda vilivyowasilishwa ndio hapo anachaguliwa kupewa ile tenda.

Kigezo kikubwa kwa tenda yenye *finance* tunachagua kigezo chenye thamani ambayo ina uwezo wa Serikali kuweza kutekelezwa. Kwa hivyo vigezo kamili vimefuatwa kama inavyofuata sheria ya *tender* na kama ilivyo sheria na taratibu za *tender* ndio zilizompeleka yeye achaguliwe kufanya hiyo kazi.

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize suali dogo sana la nyongeza.

Kwa sababu tumezoea kusikia kuwa tayari hasara imepatikana na hatua hazichukuliwi kutokana na hawa wakandarasi wengi, lakini kwa maana ile ile inasemekana sana kuna *potion* kubwa ya tatan ile, imeharibika ni nini tamko la Serikali.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ni kweli Serikali imepata hasara na taratibu za kufanya zipo na mkandarasi huyu taratibu zake zimeanza kufuatwa, kwa sababu yeye ameitengenezea hasara Serikali, hatua ya kwanza ni kumsitisha na kumsimamisha kufanya kazi hiyo. Kwa hivyo hatua

zinazofuata ni kuanza kuchukua hatua ambazo zitaonekana namna gani anaweza kuweza kuwajibika kwa hii hali ya hasara aliyoitia. Ahsante sana.

**Mhe. Spika**: Ahsante tumemaliza kuhusu utaratibu, Mhe. Mohamed Said Mohamed.

**Mhe. Mohamed Said Mohamed:** Mhe. Spika, kuhusu utaratibu Mhe. Waziri alipokuwa akijibu hakujibu suala langu la kuwa *portion* kubwa ya tatan kuwa imeharibika, tamko la Serikali.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mohamed Said Mohamed samahani kanuni gani unayotumia.

**Mhe. Mohamed Said Mohamed:** Kifungu cha 58. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu hakujibu suali langu la nyongeza linalohusu *portion* kubwa ya tatan kuharibika, nilikuwa nataka anijibu ni tamko gani Serikali inatoa kuhusu hiyo *portion* kubwa ya tatan iliyoharibika.

**Mhe. Spika:** Labda nipate maelezo kidogo kutoka kwa Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Nataka kumthibitishia Mhe. Muwakilishi kwamba sehemu iliyoharibika kama ilivyoelezwa katika jibu la kwanza ni sehemu ndogo ya magoli na *area* D ya ule uwanja; ni sehemu mbili. Na sehemu kubwa imetengenezwa vizuri na ndio maana tukasema tunatizama hatua gani za kumchukulia mkandarasi yule kwa sababu kuna sehemu amefanya vizuri na kuna sehemu ambazo zilizoharibika, na sababu zilizomsababisha kuharibika ile sehemu ilikuwa ni kuweka lami wakati wa mvua. Kwa hivyo mvua ndio iliyosababisha kuonesha kiwango ambacho hakikukamilika.

Hivyo basi Mheshimiwa aelewe kwamba ile sehemu ndogo kwa sasa hivi taratibu zinafanywa kuweza kuikamilisha na jana tulikuwa tuanze hiyo kazi, lakini tatizo kubwa la mvua limejitokeza tena. Waliokuwa hawana taarifa juzi Pemba siku ya Jumatatu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alitembelea uwanja ule na alipofika pale alikumbana na mvua, kwa hivyo kazi iliyokuwa ifanyike hiyo ndogo ya kuimalizia haikufanyika kwa mvua. Inatarajiwa kuanza punde tu hali ya jua inapokuwa vizuri na muda mfupi kabla ya mwezi wa sita tatan hiyo itakuwa imekamilika na inaanza kutumika kama ilivyotarajiwa.

**Nam. 11**

**Ujenzi wa Barabara Chambani**

**Mhe. Bahati Khamis Kombo** - Aliuliza:

Serikali inastahiki pongezi kwa kujengwa barabara ya Kenya Chambani. Hatua kubwa imefikiwa lakini barabara hii imefika Ukutini kwa Mtora tu, haikufika Matele na Chwale, pia barabara hii ina milima, kona, na ni nyembamba. Na Wambaa kwa Azani mpaka Hoteli hawana bararaba. Kutoka Kenya Chambani imekuwa kero kwa wanaokwenda kwa miguu na vyombo vidogo vidogo, kwa sababu ina magari mengi na makubwa.

Je, Serikali itatusaidia vipi wananchi wa Jimbo la Chambani ili kuondokana na shida hiyo ya usafiri.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 kama ifutavyo:-

Mhe. Spika, barabara ya Kenya Chambani ni moja kati ya barabara zilizojengwa Kusini Pemba kwa kutumia mradi uliofadhiliwa na Serikali ya Norway mwaka 2009. Katika mradi huu ulitumia mfumo wa aina mbili ya ujenzi ambao ni '*Basic Access'* na '*Secondary Economics'*. Kwa barabara zote zilizotumia *basic acess* zilikuwa upana mita 3.5, mabega ya miteremko mikali ilizingatia mfumo huu. Aidha, ziliwekwa sehemu za kupishana magari '*passing bays'*. Mfumo huu wa ujenzi ulitumika pia katika barabara za Chanjamjawiri - Tundauwa, Chanjaani – Pujini, Mzingani – Wambaa pamoja na hii ya Kenya – Chambani. Aidha, kulingana na '*design'* ya barabara hiyo ilizingatiwa sana '*Sight Distance'* katika barabara ambazo kuna milima na ndio maana mpaka leo hii tunamshukuru Mungu bado hakuna ajali yoyote iliyotoke kwenye barabara hiyo.

Mhe. Spika, katika hatua nyengine Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ina mpango mkuu wa kuziunganisha barabara za ukanda wa mashariki (kutoka Kaskazini Pemba hadi Kusini Pemba) kwa kujenga barabara ya Ole – Kengeja mradi ambao unaendelea hivi sasa ambao baada ya kukamilika utaunganisha vijiji vya Ole, Vitongoji, Pujini, Chambani, Ukutini, Chwale, Matale, Kiwani, Kendwa mpaka kufikia Kengeja.

Mhe. Spika, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba barabara ya Wambaa kwa Azani mpaka hotoli haijatengenezwa katika kiwango cha lami lakini Wizara ya Ujenzi ilifanya matengenezo ya barabara hiyo ili iweze kupitika na katika mwaka wa fedha 2013/2014 barabara hiyo ilifanyiwa matengenezo ya dharura.

**Mhe. Bahati Khamis Kombo:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa sababu barabara ambayo imetoka Ole kuelekea Kengeja ile barabara imeambatana na jimbo la Chambani pamoja na kiwani, tukiangalia sana barabara ile kutoka shehia ya Dodo kuja katika kijiji kimoja kinachoitwa Mtakamaji, Shehia ya Chambani Tumbini kuelekea Shangini, Ukutini kuelekea Milima Mikubwa miwili iliyopo katika kijiji cha Ukutini daraja la kwa Kichwa; ile sehemu ni mbaya sana. Ningeshauri Mhe. Waziri zile sehemu ambazo ni mbaya sana zikafanyiwa matengenezo ya awali.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa naomba umuulize suali.

**Mhe. Bahati Khamis Kombo:** Mhe. Waziri umejipanga vipi kuhusu sehemu zile kuzisaidia wakati wa mvua.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Spika, Wizara yetu ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji tumejipanga katika kuhakikisha tatizo hili tunalitatua. Kwa bahati nzuri mimi nilitembelea barabara hii na hizi sehemu alizonambia ni kweli tumeziona ni korofi hasa hapa Kwatumbo ambapo ni karibu na mpakani na Chonga, pale tutafanya utaratibu wa kufukia mawe kwanza na baadae kutia kifusi na kuweka *grade* pamoja na kufanya *sewage*. Kwa hiyo, mimi namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba zile sehemu korofi zote tunazifanyia utaratibu wa kuzitengeneza kwa haraka kwa mujibu wa taratibu zetu tunaita wenyewe *routing*. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Mussa Foum Mussa:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, barabara ya Kenya/Chambani ni barabara ambazo zimejengwa si muda mrefu sana, lakini barabara hii imeanza kubomoka.

Je, Mhe. Naibu Waziri, una mpango gani wa kuifanyia matengenezo ili isijemalizika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Spika, ni kweli kwamba barabara hizi za Mradi wa *NORAD* sasa hivi zina matatizo kidogo na hii imetokana na lami tuliotumia wakati ule ilikuwa inaitwa lami ya baridi na lami hii tulikuwa tunaifanyia majaribio baada ya kuwaahidi wenzetu wa Kenya na Msumbuji. Kwa hivi sasa tulituma timu yetu ya wataalamu kwenda kuangalia zile sehemu zilizopata matatizo na tumesema kwamba hizi sehemu tunazifanyia matengenezo kwa haraka ili kuilinda barabara hii isiharibike zaidi.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Mhe. Spika, ahsante kutokana na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kutokana na jitihada za serikali kuwatengenezea wananchi wake barabara ili kuondokana na usumbufu wa usafiri, wananchi wa Jimbo la Ziwani njia ya Pembeni/Mchanga wa Kwale ni kwamba ile njia haipitiki, hivyo wizara yako ina jitihada gani ya kuondosha usumbufu kwa wananchi wale ili wapate usafiri na wao wajisikie katika nchi yao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Spika, ni kweli njia ile na mimi pia nimeitembelea nimeiona kama haipitiki, lakini kama nilivyojibu hapo mwanzo kwamba hizi barabara nyengine zitakuwa katika Halmashauri ya Wilaya husika, sisi tutashirikiana na Halmashauri ya Wilaya husika katika kuhakikisha kwamba zile barabara zinazoenda katika sehemu zenye mazao zaidi tuzifanyie utaratibu wa kuzirekebisha. Pia, nimefurahishwa sana na ari kubwa ya wawakilishi wetu juu ya kutaka kushirikiana na sisi katika kuhakikisha kwamba barabara hizi zote zinapitika kwa wakati wowote ule.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, maswali yamemalizika na muda bado tunao, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kuwatangazia wageni ambao wamefika hapa leo. Wageni tulionao ni wageni wa Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Jang'ombe na ni Kikundi cha G1 Mapinduzi Kwanza. Naomba wasimame pale walipo, na wanaongozwa na Makamu Mwenyekiti wa kikundi hicho Bwana Ramadhani Ali Kimara. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tumekubaliana kwamba leo tutamwita Mhe. Waziri ili aweze kuanza kutupa majumuisha ya bajeti. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii sasa kumkaribisha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ili sasa aweze kutoa majumuisho kuhusiana na bajeti. Karibu Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima na kutuwezesha kukutana leo hii tukiendelea na kikao chetu muhimu cha bajeti.

Pili, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru na kukupongeza wewe Mhe. Spika na kumpongeza Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza letu hili kwa ufanisi na mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, nawashukuru wajumbe wote wa Baraza waliochangia na wale ambao hawakupata fursa ya kuchangia kwa umoja wao wa kuunga mkono taarifa ya hali ya uchumi na mwelekeo wa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2016/2017 na Bajeti ya Serikali kwa maana ya mapato na matumizi kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika, lazima nikiri kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wametoa michango makini, michango yenye kina, michango yenye *substance* iliyodhamiria kujenga na kutoa manufaa kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, kutokana na muda nilionao sitoweza kutoa ufafanuzi wa michango yote na hoja zote zilizotolewa, hivyo, nitawaomba wale Waheshimiwa Wajumbe, ambao michango yao sitoigusa moja kwa moja waridhike na ufafanuzi nitakaoutoa, lakini pia wajue kwamba wizara zitakapowasilisha hotuba zao za bajeti zitatoa ufafanuzi wa kina katika maeneo mbali mbali…

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri wa Fedha, samahani kabla hujaendelea naomba nimpishe Mhe. Naibu Spika, kwenye kiti halafu baada ya hapo utaweza kuendelea. Mhe. Naibu Spika, tafadhali.

*(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)*

**Mhe. Naibu Spika:** Tuendelee Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Naibu Spika, niruhusu niwatambue wale wote waliochangia katika taarifa ya hali ya uchumi na mwelekeo wa mpango wa maendeleo na bajeti ya serikali kwa mwaka 2016/2017. Waheshimiwa, waliochangia ni 31 ambao ni kama ifuatavyo.

1. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Mhe. Hamza Hassan Juma. Kupitia hotuba yake iliyosomwa kwa niaba na Mhe. Machano Othman Said.
2. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
3. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali
4. Mhe. Simai Mohammed Said
5. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
6. Mhe. Shehe Hamad Mattar
7. Mhe. Suleiman Sarahani Said
8. Mhe. Rashid Makame Shamsi
9. Mhe. Shamata Shaame Khamis
10. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
11. Mhe. Mihayo Juma N'hunga
12. Mhe. Said Omar Said
13. Mhe. Omar Seif Abeid
14. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
15. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
16. Mhe. Panya Ali Abdalla
17. Mhe. Mussa Ali Mussa
18. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
19. Mhe. Asha Abdalla Mussa
20. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
21. Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira)
22. Mhe. Miraji Khamis Mussa
23. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
24. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji 25.Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
26. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ
27. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
28. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
29. Mhe. Naibu Waziri wa Afya

Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni;

30.Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, na
31.Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

Mhe. Naibu Spika, mengi ya michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe, ililenga kutushauri juu ya mambo mbali mbali ikiwemo namna bora ya kuongeza mapato na kudhibiti matumizi ya fedha za serikali na kuwa na bajeti inayotekelezeka. Aidha, wapo Waheshimiwa Wajumbe, waliotushauri serikali zetu mbili kukaa pamoja kuona jinsi gani tunaweza kudhibiti bei za bidhaa nchini na kudhibiti kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Kimarekani. Lakini pia kukaa pamoja kwa ajili ya kutafuta fursa za ajira kwa vijana nchini. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wote kwamba ushauri wao tunauchukua na tutaufanyia kazi kikamilifu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla sasa naomba nitoe maelezo juu ya hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe kama ifuatavyo. Naanza na suala la ajira.

Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa niaba ya Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi alitaka maelezo kuhusu jinsi tulivyoweza kutatua tatizo la ajira kwa mujibu wa malengo ya MKUZA II na Dira ya Maendeleo 2020.

Mhe. Naibu Spika, suala la ajira bado ni changamoto katika nchi yetu, kwani kwa mujibu wa sensa ya idadi ya watu ya mwaka 2012 vijana wenye umri kati ya miaka 15-35 ni asilimia 36 na watoto waliochini ya umri wa miaka 15 ni asilimia 42.5. Hivyo, idadi ya watu wote waliochini ya umri wa miaka 35 ni asilimia 78 ya watu wote. Hii ni idadi kubwa ambayo inahitaji mipango madhubuti ya kukuza fursa za ajira nchini.

Aidha, suala la kutatua tatizo la ajira si la muda mfupi, serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha sekta za huduma, sekta ya kilimo na viwanda ili kuongeza fursa za ajira kwa vijana ikiwemo kuwapatia vijana wetu elimu ya amali na mikopo ili waweze kujiajiri. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumeweza kuzalisha ajira zipatazo 25,019, kati ya hizo ajira 18,539 zilipatikana katika sekta binafsi na ajira 6,480 zilipatikana serikalini.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la kusita utoaji wa boti kwa wavuvi wadogo wadogo, naomba kueleza kwamba bodi nyingi zilitolewa kwa wavuvi wadogo wadogo Unguja na Pemba kupitia Mradi wa *MACEMP* uliokuwa ukipata

ufadhili wake kutoka Benki ya Dunia. Mradi huo ulitekelezwa katika kipindi cha mwaka 2007-2010 na kwa sasa mradi huu umemalizika. Hata hivyo, serikali imeandaa *programme* ya kuendeleza uvuvi katika bahari kuu na tayari imetiliana saini na Kampuni ya Hairu ya Sri Lanka kwa ajili ya kushirikiana kusaidia vijana wetu kuingia katika uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Naibu Spika, katika bajeti hii serikali pia imepanga kununua boti kwa ajili ya kuwapatia vijana kuweza kuvua katika bahari yenye maji mengi, ikiwa ni sehemu ya mpango wa kuendeleza ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba ya Kamati ya Wenyeviti ilielezwa suala la kusita kwa zoezi ufungaji wa mita za maji katika maeneo ya biashara.Mhe. Naibu Spika, naomba kuwaeleza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwamba zoezi la kufunga mita katika maeneo ya biashara halijasita bado linaendelea na tayari maeneo ya Pwani Mchangani, Matemwe na maeneo ya Mjini Magharibi yameshafungiwa mita hizo.

Mhe. Naibu Spika, katika sekta ya afya ushauri wa kuanzisha kitengo maalum cha kutengeneza vifaa vya watu wenye ulemavu. Kwa mfano, miguu bandia tumeusikia na wizara inayohusika italizingatia suala hili. Aidha, suala la kutafuta eneo jengine kwa ajili ya kambi ya wagonjwa wa kipindupindu tayari suala hili limetolewa ufafanuzi wa kina na Mhe. Naibu Waziri wa Afya na naamini maelezo aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri wa Afya, yametosheleza kutoa ufafanuzi juu ya hoja hiyo.

Mhe. Naibu Spika, katika sekta ya elimu ni kweli hali ya urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu si ya kuridhisha, suala la kuangalia namna bora ya utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo litazingatiwa na wizara husika kama ilivyoshauriwa na Mhe. Mwakilishi, aliyeuliza suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mfumo mpya wa elimu ambao unamtaka mwanafunzi anayemaliza darasa la 6 kuendelea moja kwa moja darasa la 9. Naomba kueleza kwamba mfumo huu unatokana na Sera ya Elimu ambayo tumeipitisha wenyewe na iliyoandaliwa kwa kushirikisha wadau mbali mbali.Kupitia mfumo huu inatarajiwa mtoto ataanza darasa la kwanza akiwa na umri wa miaka 6 na atamaliza darasa la sita akiwa na umri wa miaka 11, na kumaliza darasa kumi na mbili akiwa na umri wa miaka 15, hivi sasa kuufanyia tathmini mfumo huu ni mapema sana. Hata hivyo, sekta inayohusika imesikia ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe na watauzingatia kwa wakati muafaka. Tathmini hii wakati itakapofanyika vile vile itasaidia kutoa mapendekezo juu ya mitaala ya elimu ya amali.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati za Wenyeviti pia walitaka kujua ni skuli ngapi Unguja na Pemba zina skuli za maandalizi na ngapi hazina skuli hizo. Mhe. Naibu Spika, zipo skuli 30 zinazotoa elimu ya maandalizi pekee kwa maana *primary*, aidha, skuli 154 kati ya skuli 380 za serikali zinazotoa elimu ya msingi nazo zina madarasa ya elimu ya maandalizi. Vile vile, vipo vituo 304 vya tucheze tujifunze kwa maana (TUTU) jumla ya wanafunzi 55,781 wapo katika elimu ya maandalizi sawa na asilimia 58.2 ya watoto wote walio katika umri wa kuwa katika elimu hii ya maandalizi.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli tumekuwa tukipata matatizo ya mara kwa mara ya mafuriko hapa nchini hususan katika miaka ya hivi karibuni. Mwaka huu tulipata tatizo hilo na mwaka jana vile vile tulipata tatizo hilo na ni kweli wenzetu wanaopata matatizo ya kuingiliwa na maji katika majumba yao huwa wanafadhiliwa katika Skuli ya Mwanakwerekwe "C" jambo ambalo limekuwa likileta usumbufu kwa wanafunzi na walimu wa skuli hiyo.

Mhe. Naibu Spika, katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hili serikali imeandaa Kanuni ya Usimamizi na Udhibiti wa Ardhi Zanzibar na imepitishwa rasmi mwaka 2015. Kanuni imeweka mfumo imara wa utoaji wa vibali vya ujenzi na ipo kamati ambayo inasimamia masuala haya ambayo yanawashirikisha Wajumbe kutoka Baraza la Manispaa, Wajumbe kutoka Halmashauri "A" na "B", Wajumbe kutoka Mamlaka ya Mji Mkongwe, Bodi ya Watalamu wa Ujenzi na Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wakulima na Wenye Viwanda. Kwa hivyo, suala kubwa ni udhibiti wa ujenzi katika maeneo yanayotuama maji, maeneo ya njia za maji ambalo kamati hii itaendelea kufanya kazi zake ili kuhakikisha kunakuweko na udhibiti katika ujenzi holela.

Mhe. Naibu Spika, aidha, kupitia Mradi wa Huduma za Mji (*ZUSP*) serikali inaendelea kujenga misingi ya maji ya mvua katika maeneo mbali mbali ya mji kwa ajili ya kuondoa tatizo la kutuama kwa maji na kufurika katika maeneo ya makaazi. Katika mpango wa dharura kwa maana ya *emergency preparedness*, serikali tayari imeziweka skuli 21 ambazo zinaweza kutumika wakati wa dharura kwa Unguja na Pemba, lakini skuli hizi zinatumika pale kunapotokea dharura tu.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza imetoa ushauri kuhusu uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine za kutolea risiti *EFD* na kuachana na mfumo wa kukusanya fedha taslim kwa maana ya *cash* ikiwa pamoja na *ZRB* na *TRA* kukaa pamoja. Ushauri huu ndio hasa unaotaka kutekelezwa na serikali kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017. Serikali itaanza

utekelezaji wa matumizi ya mashine za risiti na kuyagawa maeneo kwa ajili ya ukusanyaji kodi na kuwatambuwa walipa kodi wote ambao watakaotambulika na *ZRB* na *TRA*. Tunahisi mpango huu utarahisisha ukusanyaji wa mapato lakini vile vile kuongeza mapato ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, serikali katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 itaweka mkazo maalum wa kufuatilia vyanzo vyote vya mapato ikiwemo kupata taarifa sahihi za wageni wanaoingia nchini na ukaguzi wa vibali vya kazi kwa wageni wanaokuja kwa ajili ya kufanya kazi nchini. Naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba hatutomvumilia mtendaji yeyote atakayesababisha upotevu wa mapato ya serikali. Aidha, serikali itafuatilia na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria wafanyabiashara na watoa huduma wote ambao wanastahiki kulipa kodi na ambao watakwepa kulipa kodi kama inavyotakiwa. Kama wapo wanaowashawishi watu hao kutokulipa kodi wajue kwamba wanakwenda kinyume na sheria za nchi na hatua zitachukuliwa zidi yao kwa wale watakaobainika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu pendekezo la kufanyiwa ukaguzi maalum Bodi ya Mapato (*ZRB*), kuhusiana na ukusanyaji wa mapato naomba kuwaeleza waheshimiwa kwamba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) anafanya kazi zake bila ya kuingiliwa na taasisi yoyote au mtu yeyote, anafanya kazi kwa kukagua taasisi zote za serikali na mashirika ya umma kwa kila mwaka. Hivi sasa *CAG* anaendelea na ukaguzi wa kina kwa hesabu za mwaka 2014/2015 katika taasisi mbali mbali za serikali. Hivyo, pindi ikionekana ipo haja ya kufanyiwa ukaguzi maalum kwa Bodi ya Mapato uwezo huo Mheshimiwa *CAG* anao na jambo hilo linaweza kufanyika wakati wowote.

Mhe. Naibu Spika, wazo la Mhe. Hassan Khamis Hafidh la kuanzisha wakala kwa ajili ya ufuatiliaji wa mapato ya serikali litafanyiwa kazi na hatua muwafaka zitachukuliwa pindi ikionekana ipo haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia imependekeza vianzio vya mapato mbali mbali na mikakati ya kuimarisha makusanyo ya mapato mfano maeneo ya maegesho, wizara yangu itaviangalia na kuvitathmini vianzio vilivyopendekezwa na kuchukua hatua muwafaka pale itakapohitajika.

Mhe. Naibu Spika, katika kupunguza upotevu wa mapato yanayotokana na matumizi ya umeme kwa wateja, shirika linaendelea kufanya uhakiki wa wateja wake na kuongeza matumizi ya mita za TUKUZA pamoja na kutoa huduma kwa wateja juu ya namna bora ya kutumia huduma za umeme na kufanya malipo stahiki kwa wakati.

Sambamba na hilo shirika linatoa taaluma juu ya kuwepo kwa fursa za mikopo kwa ajili ya kuungiwa umeme kwa wananchi wa visiwa vyote vya Unguja na Pemba. Hivyo, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tunaomba tuwashajihishe wananchi wetu wale ambao watahitaji huduma za mikopo kwa ajili ya kuungiwa umeme basi wafike katika Shirika la Umeme na huduma hiyo itatolewa bila ya matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ada ya abiria wanaosafiri kwa ndege kuongezwa kutoka shilingi 2,000 na kuifanya isilingane na ile wanayotozwa wasafiri wa boti, jambo hili lilijadiliwa hapa hapa Barazani na kukubaliwa kutumia viwango hivi kwa wasafiri wa ndege na boti na iwapo Waheshimiwa Wajumbe hivi sasa wanaona ipo haja ya kutofautisha viwango hivyo baina ya usafiri wa ndege na wale wanaotumia boti serikali italizingatia jambo hilo katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, liliulizwa suala la *share* za serikali katika Kampuni ya Simu ya *ZANTEL*. Kwanza napenda kusema kwamba kampuni hii mwanzo ilikuwa inamilikiwa na Kampuni ya *Et El Salat* pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa *share* ya asilimia 85, asilimia 15. Ile asilimia 85 ilikuwa *Et El Salat* na asilimia 15 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *Et El Salat* wameuza *shares* zao zote kwa Kampuni ya *Millicom* kwa maana ya asilimia 85 na kwa hiyo hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imebaki na *share* yake ile ile ya asilimia 15.

Mhe. Naibu Spika, tunapokea ushauri wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kufanya tafiti za viwanda vinavyoweza kuanzishwa kupitia kitengo cha *PPP* vikiwemo viwanda vya samaki na kusindika mwani, sambamba na kuhamasishwa wawekezaji kuwekeza katika viwanda hivyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumshukuru sana Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Mhe. Mohamed Ahmada, kwa maelezo yake ya kina kwa hoja zote zilizotolewa katika sekta ya mawasiliano na usafirishaji. Ni imani yangu kuwa Waheshimiwa Wajumbe wameridhika na maelezo yaliyotolewa kwa ufasaha na kwa kina na Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu deni la Dola za Kimarekani 9.4 milioni linalodaiwa na mjenzi wa barabara za Pemba zilizojengwa kupitia ufadhili wa *BADEA* na *Saud Fund*, Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji inaliangalia deni hilo na kulihakiki na kujua ni kiasi gani hasa mkandarasi huyo anastahiki kulipwa ili hatua za kuanza

kumlipa zianze kuchukuliwa. Tutachukua hatua za haraka ili kuhakikisha uhakiki huo unakamilika kwa wakati na mkandarasi huyo kuweza kulipwa kile anachostahiki.

Mhe. Naibu Spika, tuipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuanzisha pencheni ya wazee. Zanzibar imetangulia nchi nyingi za Afrika kuwa na pencheni hii na ni ya mwanzo kwa nchi za Afrika Mashariki kuanzisha pencheni ya wazee. Hadi sasa utoaji wa pencheni ya wazee unaendelea vizuri wizara inayohusika imekusanya taarifa zote muhimu za wazee hao kwa maana ya *database* kama livyoshauriwa na itaendelea kuzi-*update database* ama kwa kuwatoa wale watakaokuwa hawastahiki kwa sababu mbali mbali na kuwaingiza wale ambao wanastahiki.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu malipo ya viinua mgongo napenda kulieleza Baraza lako tukufu kwamba Wizara ya Fedha na Mipango tayari imejiandaa kuendelea kulipa madeni ya viinua mgongo kwa kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu. Fedha zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kuendeleza malipo hayo.

Mhe. Naibu Spika, ilikuja hoja ya serikali kuandaa bajeti yenye uhalisia na kwa hapa Mhe. Naibu Spika, napenda kueleza kwamba bajeti inaandaliwa kutokana na viashiria vya mapato na upatikanaji wa misaada, ruzuku na mikopo na matumizi hupangwa kwa mujibu wa matarajio ya upatikanaji wa fedha hizo. Ruzuku na mikopo inayoingizwa katika bajeti ni ile tu ambayo wafadhili wameshatoa dhima ya kutoa fedha hizo kwa maana ya *commitment.* Kwa kawaida nakisi ya bajeti huwa inaoneshwa ambayo pia inazibwa kupitia mikopo ya ndani wakati wa utekelezaji. Hata hivyo, zipo changamoto ambazo hujitokeza na wakati mwengine huwa tunashindwa kuzitabiri. Kwa mfano, kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi au kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, suala la Bima ya Afya kwa watumishi wa umma nalo liliulizwa na Waheshimiwa Wajumbe. Naomba niseme tu kwamba suala hili linaendelea kufanyiwa kazi kupitia timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Shirika la Bima, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Wizara ya Afya na Idara ya Utumishi Serikalini. Mara baada ya kukamilika kwa kazi yetu hii ripoti itawasilishwa serikalini kwa mazingatio yanayofaa. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba suala hili ni kweli limechukua muda mrefu lakini tutajitahidi kulisimamia kuona kwamba suala

hili linamalizika haraka iwezekanavyo na mapendekezo yanawasilishwa serikalini. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele Mhe. Ali Suleiman Ali, alitoa ushauri juu ya utoaji wa risiti katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato na alitaka serikali kuliangalia tatizo la maji na upatikanaji wa umeme katika Jimbo la Kijitoupele. Lakini pia suala kama hili lilielezwa na Waheshimiwa Wajumbe wengine kwa mfano Mhe. Asha Abdalla Mussa wa Kiwengwa walizungumza masuala ya maji na wengine vile vile katika maeneo tafauti.

Niseme tu kwamba maelezo yao tumeyasikia, ushauri wao tumeupokea na sekta zinazohusika zitayachukua na kuyafanyia kazi kwa mujibu wa hali itakavyoruhusu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammedraza Hassanali, alitaka fedha zilizotengwa kwa ununuzi wa vifaa zipelekwe katika barabara za ndani. Wazo hili pia liliungwa mkono na Mhe. Mihayo Juma N'hunga la kupunguza fedha hizi na kutumika katika maeneo muhimu.

Mhe. Naibu Spika, suala hili lilifafanuliwa vizuri sana na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, na ni matumaini yangu kwamba maelezo yake yametosheleza kujibu au kutoa ufafanuzi wa hoja iliyotolewa.

Kuhusu suala la gawio la *BoT* la asilimia 4.5 ni kweli suala hili lilikuwa la muda na jibu la suala hili limo katika mapendekezo ya Tume ya Ripoti ya Tume ya Pamoja ya Fedha yaliyotoa vigezo vya jinsi ya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano, baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ripoti hiyo bado inaendelea kufanyiwa kazi na pande mbili za Jamhuri ya Muungano. Niseme tu kwamba tutalifuatilia na kuona pia maoni yale yanazingatiwa vizuri na pande zote mbili na muwafaka unapatikana juu ya suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la uhaulishaji wa *VAT*, maana ya *VAT Refund* kutoka Tanzania Bara kwa bidhaa zilizozalishwa Zanzibar na kutumika Tanzania Bara, suala hili tayari limeshapata ufumbuzi na SMT hivi karibuni itaifanyia marekebisho sheria mpya ya *VAT* ili kurudisha utaratibu wao wa awali wa SMT kuendelea kuwa wakala wa *VAT* na kufanywa Tanzania Bara kwa bidhaa zilizozalishwa Zanzibar na kuuzwa. Hadi mwezi Aprili, 2016 Zanzibar ilitarajiwa kupata jumla ya shilingi 17.5 bilioni kupitia mpango huu. Nina furaha kusema kwamba muda wowote kuanzia sasa tunatarajia kupata

shilingi 12.5 bilioni na zile fedha nyengine zilizobaki zitafuatiliwa ili ziweze kupatikaa hapo baadae. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha ipo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 133 hadi kifungu cha 134 na kuwekewa utaratibu katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Toleo la 2010 kifungu cha 114 hadi 115. Aidha, tume hii imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Jamhuri ya Muungano, Sheria ya Tume ya Fedha za Pamoja ya mwaka 1996. Katika mwaka 2016/2017 tume hii imeweza kukaa mara nne na itaendelea kukutana kujadili mambo mbali mbali yanayohusi mahusiano ya fedha baina ya serikali zote mbili.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Simai Mohammed Said, naye alitaka ufafanuzi katika masuala mbali mbali ikiwemo aina ya matamasha na maonesho ya kibiashara. Mhe. Naibu Spika, masuala ya maonesho na matamasha ya kibiashara yamo katika programu mjumuisho ya kuendeleza utalii ikiwa pamoja na kufanya utafiti wa hali ya utalii na biashara katika visiwa vidogo vidogo vya Fundo, Kokota, Njao, Bawe na *Prison Island*. Nakubaliana na Mhe. Simai Mohammed, kuwa filamu pamoja na sanaa mbali mbali nazo ni sehemu ya vivutio vya utalii na vinachangia katika kukuza mapato na hivyo iko haja ya kuendeleza sanaa...

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri, Mhe. Simai, ameleta marekebisho ya jina lake nafikiri halikuandikwa sawa sawa, jina lake ni Mhe. Simai Mohamed Said. Naomba ufanye marekebisho hayo.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Sawa sawa Mhe. Naibu Spika, nachukua, Mhe. Simai Mohamed Said. Mhe. Naibu Spika, vile vile, napenda kumfahamisha Mhe. Simai Mohamed Said, kuwa deni la serikali linaripotiwa kwa shilingi ila kwa wakati wa kufanya malipo malipo hayo hufanyika kwa sarafu iliyokubaliwa katika mkataba. Aidha, ushauri wake wa kuangalia suala la uondoaji wa *visa* wakati wa msimu mdogo wa utalii na kuyaalika makampuni ya kimataifa kuja kuwekeza katika maeneo haya ya uwekezaji ya Fumba na Micheweni tunaufufua na tutauzingatia.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la kuwa na nishati mbadala ikiwa ni njia ya kujitayarisha na kuongezeka kwa mahitaji ya nishati, suala hili limo katika hatua za utafiti ambao utafiti huo upo katika hatua za mwisho kukamilika.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Simai Mohamed, pia alizungumzia kuhusu suala la Sheria ya Manunuzi kufanyiwa marekebisho.Naomba kumjuilisha kwamba

sheria hii hivi sasa imo katika hatua za mwisho kufanyiwa marekebisho na hivi karibuni itawasilishwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu kwa ajili ya kupata maoni yao kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, Mhe. Simai, alizungumzia kuhusu suala la safari za kikazi nje ya nchi na kusema kwamba watumishi wasibanwe kwenda katika safari hizi. Mhe. Naibu Spika, naomba ifahamike kwamba safari za kikazi nje ya nchi hazijafutwa wala hakuna mfanyakazi aliyekatazwa kusafiri. Kinachotakiwa ni kwamba pale fedha za serikali zinapotumika basi safari hizo lazima tujiridhishe sisi wenyewe kwamba safari hizo zitakuwa na tija na manufaa kwa nchi yetu.

Lakini vile vile kuhakikisha kwamba kama safari inatosheleza kwenda mtu mmoja au wawili hakuna haja ya kwenda watu watano. Kwa hiyo, ni suala la ufanisi katika kutafuta safari hizo. Jambo hili halina ubaya na utaratibu uko wazi wa kuomba kibali cha kusafiri nje kwa viongozi na watendaji katika ngazi mbali mbali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, maoni yalitolewa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Mwakilishi wa Jimbo la Chaani la kuanzisha viwanda vya kusindika samaki na kuendelea kukaa na sekta binafsi. Ni ushauri mzuri na ushauri huu tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Suleiman Sarahan Said, nao walizungumzia juu ya masuala mbali mbali yakiwemo bima ya afya, kuendeleza sekta ya kilimo, wananchi kuunganishwa na huduma ya umeme, kumaliza madeni ya kiinua mgongo, kuimarisha utendaji wa mashirika ya serikali. Kwa kweli ushauri wao ni mzuri na serikali kwa maana ya sekta zinazohusika wameusikia na wataufanyia kazi. Aidha, Mhe. Suleiman Sarahan, alitaka Meli ya *MV.* Mapinduzi isikodishwe na kutaka kuimarisha makusanyo ya mapato kwa kutumia mashine za risiti katika maeneo ya maegesho ya magari.

Serikali haina mpango wa kuikodisha Meli ya *MV.* Mapinduzi, lakini vile vile ushauri wake wa kuimarisha mapato katika maegesho ya magari sambamba na kukamilishwa kwa jengo la abiria katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume na kuwa na ramani za ujenzi wa barabara katika mji wetu ili kuepusha ujenzi holela, kujenga skuli zenye viwango na kuendelea kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia haya yote tunayachukua ni ushauri mzuri Mheshimiwa na tutaufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Mhe. Rashid Makame Shamsi, alitaka suala la utoaji pencheni kwa wazee liangaliwe vizuri. Kama nilivyosema mwanzo suala hii linasimamiwa vizuri liko kwenye mikono mizuri ya Wizara ya Uwezeshaji na asiwe na wasi wasi na *inshaalla* Mwenyezi Mungu atatujaalia litakwenda vizuri na alieleza kwamba suala la manunguniko ya baadhi ya wafanyakazi juu ya kuanza mishahara mipya mwezi wa Aprili mwakani.

Suala hili pia lilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengine na napenda nasema tu kwamba kuhusu suala hili ni vyema ikaeleweka kwamba hii si mara ya kwanza kwa mishahara kutangazwa na utekelezaji kuanza miezi inayofuata. Imefanyika mara nyingi katika miaka tisini na ni utaratibu wa kawada, na pia Mhe. Rais nataka niseme kwamba alipotoa kauli ya kuongeza kima cha mshahara kutoka laki moja hamsini elfu hadi laki tatu alisema utekelezaji wake utaanza ndani ya mwaka wa fedha wa 2016/2017. Mhe. Rais hakusema ni mwezi gani tutaanza. Kwa hivyo, na mshahara huu utaanza kutolewa ndani ya mwaka wa fedha 2016/2017.(*Makofi*)

Suala la mishahara ni suala nyeti na ni miongoni mwa matumizi ya mwanzo kwa umuhimu. Hivyo, upitishaji wa mishahara unahitaji maandalizi mazuri na ya kina ili baadae kuepusha malalamiko ya wafanyakazi ambayo yanaweza kutokea.

Mhe. Naibu Spika, katika suala hili la mishahara pia naomba kutoa ufafanuzi kwamba kiliongezwa kwa asilimia moja ni kile kima cha chini. Kwa maana kutoka shilingi laki moja hamsini elfu kwenda laki tatu na isije ikafahamika kwamba kila mfanyakazi katika ngazi yoyote ataongezwa kwa asilimia mia moja. Sio hivyo wale wenye mishahara ya juu wataongezewa *proportional*, *l*akini sio kwamba wataongezewa kwa asilimia mia moja. Watakaopata asilimia mia moja ni wale wanaopata kima cha chini cha shilingi laki moja hamsini elfu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rashid Makame Shamsi, pia alizungumzia suala la bima kwa vyombo vya maringi mawili na kusema kuwa kima wanachotozwa ni kikubwa kwa vyombo hivyo kwani vyombo hivyo hutumiwa na watu masikini. Nieleze tu kwamba suala la bima linaendeshwa kwa mujibu wa misingi ya sheria na viwango vya kutoza kodi hizo vimewekwa kwa kuzingatia uhalisia pindi inapotokea ajali na inapohitaji kulipa gharama kwa upotevu wa mali na maisha. Suala hili linahitaji uelewa kwa wananchi na kwamba kima kinachotozwa iwe hamisini elfu au sitini elfu kwa mwaka sio kikubwa ikilinganishwa na faida inayoweza kupatikana kutokana na mtu kuwa na bima.

Mhe. Naibu Spika, suala la ulipaji wa fidia za majengo kwa ajili ya kupitisha mradi wa ujenzi wa misingi ya kutolewa maji ya mvua kwa maeneo yote ambayo mradi huu utapita tayari limeshapatiwa ufumbuzi na fedha kwa ajili ya kutoa fidia hiyo zimeshapatikana, tunachokifanya sasa hivi ni kukamilisha utaratibu ili fedha hizo ziweze kulipwa wale wanaostahiki kwa viwango stahiki. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, michango iliyotolewa na Mhe. Shamata Shaame Khamis na Mhe. Abdalla Maulid Diwani, tumeipokea na tutaifanyia kazi. Aidha, hoja zilizotolewa na Mhe. Mihayo Juma N'hunga, zimefafanuliwa vizuri na Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na sina haja ya kurudia.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, Mhe. Mihayo Juma N'hunga na Mhe. Hassan Khamis, walizungumzia suala la kuanzisha benki ya wanawake na benki ya vijana. Wazo hili sio baya ila Mhe. Naibu Spika, tafiti mbali mbali zilizofanywa imeonekana kuwa kuanzisha benki hizi hazitokuwa na manufaa ya moja kwa moja kwa walengwa kwani zitahitaji kuendeshwa kubiashara ili huduma zake ziweze kuwa endelevu.

Hakuna benki ambayo itaanzishwa isijiendeshe kibiashara ama itakuwa inategemea kupata ruzuku kutoka serikalini ya mara kwa mara ambalo jambo hili linawezekana ikawa kwa muda huu na kipindi hichi likawa ni suala gumu. Mahitaji yanayohitajika ili kuweza kuanzisha benki ni mikubwa lazima uwe na mtaji wa kuanzia shilingi bilioni kumi na tano ili uweze kuanzisha. Ni vyema kufikiria, hapa nilikuwa nasema na naomba kurudia ni vyema kufikiria kuanzisha dirasha maalum katika benki za biashara zilizopo kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana na wanawake. Ni suala ambalo linaweza kuendelea kujadiliwa. Lakini matokeo ya tafiti yametuonesha kwamba *feasibility* ya kuanzisha benki hizi kwa hapa Zanzibar zina changamoto zake.

Mhe. Naibu Spika, nawapongeza Mhe. Said Omar, Mhe. Omar Seif Abeid, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Mussa Ali Mussa, Mhe. Masoud Abdrahman na Mhe. Hassan Khamis Hafidh, kwa maoni na michango yao mbali mbali ambayo yote tunaichukuwa na tutaizingatia.

Aidha, naipokea michango yote iliyotolewa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Tatu Mohamed Ussi na kwa yale mambo ambayo yamegusa sekta mbali mbali, wahusika wamesikia hoja hizo na watakuja kuzitolea ufafanuzi wakati wa kuwasilisha hotuba za bajeti za wizara zao. Sekta zilizoguswa ni pamoaja na maji safi na salama, afya, miundomboni ya barabara, kilimo na usafiri wa baharini. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira) alitaka kujua

sababu za kupungua kwa idadi ya watalii walioingia nchini katika kipindi kilichoripotiwa.

Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu sababu kuu zilizopelekea kupungua kwa idadi ya watalii waliongia kwanza tishio la maradhi ya Ebola yaliyozikumba nchi za Afrika Magharibi. Lakini pia tukumbuke kwamba nchini yetu katika kipindi cha mwaka huu ilikuwa katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu. Lakini vile vile katika nchi ambazo tunategemea kupata watalii chumi zao nazo zilitetereka kwa kiasi fulani, hizo ndizo sababu kuu tatu zilizopelekea idadi ya watalii kupungua katika kipindi hichi.

Mhe. Naibu Spika, suala la Mhe. Miraji Khamis Mussa, kuhusu utoaji vibali kwa meli za uvuvi wa bahari kuu. Wizara inayohusika na suala hili tayari imelisikia na naamini italifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Zulfa Mmaka, alieleza kuwa Afisi nyingi za serikali huko Pemba zinatumia majengo ya kukodi ya watu binafsi na vile vile alitaka kujua iwapo taa za barabarani zinazoendelea kujengwa katika mji wa Zanzibar nazo zitajengwa kwa upande wa kule Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli baadhi ya Afisi zetu huko Pemba zinatumia majengo ya watu binafsi kwa njia ya kukodi. Serikali inalitambua hilo na ndio maana imeanzisha programu maalum ya ujenzi wa Afisi za Serikali kwa Unguja na Pemba. Kwa upande wa Unguja serikali tayari imekamilisha ujenzi wa Afisi ya Katiba na Sheria lililopo pale Mazizini katika mwaka fedha 2016/2017 tunarajia kuanza ujenzi wa jengo la Afisi pale Gombani Pemba ambalo litatumika na Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Uwezeshaji, Wazee Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara na Nchi, afisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Jumla ya Shilingi bilioni tano zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo hili. Lakini vile vile zipo karibu shilingi milioni mia sita ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la Wizara ya Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto kwa hapa Unguja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuhusu uwekaji wa taa za barabarani kwa Pemba, naomba kumjulisha Mhe. Zulfa Mmaka kwamba kupitia mradi huo wa *ZUSP* awamu wa pili taa za barabarani zitawekwa katika mjini yote mitatu; kwa maana mji wa Chake Chake, Mkoani na Wete na jumla ya dola za Kimarekani milioni tano nukta tano zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji kisiwa cha Pemba ikiwemo suala la taa za barabarani. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naomba kuchukuwa fursa hii kumshukuru sana Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Moh'd Shein kwa kutuamini na kutupa dhamana ya kusimamia wizara hii. Aidha, namshukuru sana Mhe. Balozi Seif Ali Idd Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa miongozo na maelekezo anayotupatia katika majukumu yetu.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Spika, na nakushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza pamoja na Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano wanayotupatia ambayo yametusaidia sana katika kufanikisha kazi zetu.

Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa michango mbali mbali katika hotuba zetu za muelekeo wa Mpango wa Maendeleo na kwa Bajeti ya Serikali mwaka 2016/2017.

Vile vile nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, kwa kusaidia kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wakati wa kujadili hotuba zao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nachukuwa nafasi hii kuwashukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango ndugu Khamis Mussa Omar, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ndugu Ali KhamisM Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango ndugu Juma ReliM Makamishna na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi kubwa walioifanya ya matayarisho ya muelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017. (*Makofi*)

Nawashukuru watendaji wote wa wizara mbali mbali za serikali na waandishi wa habari kwa mashirikiano katika kipindi chote cha kuwasilisha na katika kipindi cha majadiliano ya hotuba tulizoziwasilisha hapa Barazani. (*Makofi*)
Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri, sasa Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale ambao wanakubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2016/2017 wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Mhe. Waziri, tukuombee kwa Mwenyezi Mungu kila la kheri na mafanikio katika utekelezaji wako. Katibu.

## KAULI ZA SERIKALI

### Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mwaka 2013/2014, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirikana Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 2013/2014,Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara kwa 2014/2014 naRipoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa Kipindi cha Kuanzia 2011/2015

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uzima na afya kutuweka katika hali ya usalama na amani.

Nampongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Moh'd Shein kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana katika uchaguzi uliofanyika mwezi Machi mwaka huu. (*Makofi*)

Aidha, nachukuwa nafasi hii kukupongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuendelea kuteuliwa nafasi yake ya Makamu wa pili na kwa jinsi anavyotupa ushauri na miongozi mbali mbali shughuli zetu za kila siku.

Nachukuwa nafasi hii Mhe. Naibu Spika, kumpongeza Mhe. Spika, kukupongeza wewe Mhe. Naibu Spika, na Wenyeviti wetu kwa kuchaguliwa kwenu kuliongoza Baraza hili tukufu na kukuombeeni kwa Mwenyezi Mungu akupeni hekima busara na umahiri katika kutekeleza majuku yetu ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukuwa nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kupata nafasi ya kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuwakilisha wananchi wa Majimbo yote ya Zanzibar.

Aidha, nawapongeza Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuteuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Ali Moh'd Shein kwa lengo la kulitumikia taifa hili.

Aidha, naomba niwapongeze wale wote waliopata nafasi pamoja na mimi za uteuzi wa Mawaziri na Manaibu Mawaziri na kuwatakia kila la kheri.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukuwa nafasi hii kulishukuru Baraza la Wawakilishi lililopita kwa kuzipokea na kuzifanyia kazi Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali mwaka 2012/2013 ambapo hatua mbali mbali zilichukuliwa na Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Baraza.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima nachukuwa fursa hii kuwasilisha Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali kwa mwaka 2013/2014.

Kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali ilitekeleza majuku yake ya kikatiba kwa kukagua mahesabu ya mwaka 2013/2014 pamoja na kufanya ukaguzi yakinifu kwa mfuko wa barabara kwa Unguja na Pemba. Aidha, Afisi ilikagua hesabu za mfuko wa jimbo kwa kipindi cha miaka mitano, yaani kuanzia 2011 hadi 2015.

Matumaini yangu ripoti hizi zitafanyiwa kazi na kamati inayohusika na kuchunguza hesabu za serikali kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na utawala bora juu ya mapato na matumizi ya fedha na rasilimali umma.

Kazi za akaguzi wa mahesabu ni kazi nyeti na muhimu katika kuimarisha uwajibikaji wa matumizi ya fehda na rasilimali za umma. Kutoka na unyeti na umuhimu wa kazi hizi mambo mengi ya msingi yanahitajika ikiwemo kuwa na wataalamu katika fani mbali mbali na watendaji waaminfu pamoja na uadilifu wa hali ya juu.

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 112 cha Katiba hiyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali anawajibika kukagua Mahesabu ya Serikali ya Mapinduzi pamoja na Taasisi zake zote zilizokuwemo, zikiwemo na mashirika na mamlaka mbali mbali na kwa kutoa taarifa kukaguzi huo kwa mujibu wa katiba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 112, Sehemu ya Tatu cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kufanya wafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinakusudiwa kutolewa katika mfuko wa Hazina ya Serikali ya Zanzibar matumizi yake yameidhininishwa na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

(b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yametokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zinazohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumizi yamefanywa na kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo.

(c) Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za serikali ya Mapinduzi Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa serikali ya Mapinduzi Zanzibar, hesabu za Mahakama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vinavyohusika na Baraza la Wawakilishi.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 112, kifungu cha 5, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawajibika kuwasilisha taarifa ya ukaguzi mara atakapomaliza kufanyakazi za ukaguzi. Taarifa ambazo zinazonesha hali halisi na mwenendo mzima wa matumizi ya fedha na rasilimali za umma kwa kipindi kilichokaguliwa.

Mhe. Naibu Spika, kazi za ukaguzi wa hesabu ni muhimu sana katika kuimarisha Utawala Bora ambapo ni nidhamu na uwajibikaji wa matumizi ya fedha na rasilimali za umma huzingatiwa. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inaendelea kutoa mchango mkubwa katika kuimarisha uwajibikaji na kukuza utawala bora nchini na kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, upeo na madhumuni wa ripoti ya ukaguzi. ripoti hizi zimekusanya taarifa za ukaguzi wa mahesabu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yakiwemo Mawizara na Taasisi mbali mbali za serikali. Kwa kuzingatia taarifa za matapo na matumizi ya kawaida, matumizi ya maendeleo pamoja na michango mbali mbali kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa kipindi cha mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2014.

Aidha, kwa upande wa ukaguzi wa hesabu za Mfuko wa jimbo, ripoti hii imekusanya taarifa za ukaguzi mfuko wa maendeleo ya jimbo kwa majimbo yote ya uchaguzi wa Zanzibar. Ukaguzi huo ulijikita katika kuangalia viashiria vya maeneo hatarishi katika majimbo yaliyokaguliwa ambapo mbinu zilizotumika ziliangalia mazingira ya majimbo yaliyokaguliwa ikiwemo

mifumo na udhibiti wa ndani, na kutathmini viashiria hatarishi vitakavyoathiri udhibiti wa ndani pamoja na utekelezaji wa miradi katika majimbo hayo.

Katika ukaguzi huo imebainika kwamba miradi hiyo imetekelezwa kwa kufikia hatua tofauti kulingana na fedha iliyopatikana katika majimbo yote ya Unguja na Pemba, ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 3 zilipatikana na kutumika katika majimbo hayo katika mwaka 2011 hadi 2015.

Katika ukaguzi huo imebainika kujitokeza kwa kasoro za kiutendaji kwa baadhi ya majimbo na kupelekea kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba kulikuwa na dosari mbali mbali katika utendaji na utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo hayo. Baadhi ya dosari hizo ni kama hizi zifuatazo:-

1. Ukiukwaji wa sheria mbali mbali katika utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo Sheria ya Fedha Nam. 12 ya 2005, Sheria ya Ununuzi na Ugavi Nam.9 ya 2005 na Sheria ya Mfuko wa Maendeleo Nam. 4 ya 2012.

2. Kukosekana kwa taarifa na kumbukumbu za vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Mfuno wa Jimbo.

3. Kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

4. Kukosekana kwa kumbukumbu za hesabu pamoja na madaftari mbali mbali yanayohusiana na upokeaji, utoaji na uhifadhi wa vifaa mbali mbali vilivyonunuliwa kwa ajili ya miradi husika.

5. Kutokuelewana kwa baadhi ya Wajumbe wa Kamati na Mwenyekiti wa Kamati ambapo kumeathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo husika.

6. Kukosekana kwa mashirikiano ya kutosha baina ya Wajumbe wa Kamati kwa baadhi ya Majimbo.

**Kwa upande wa Ukaguzi Yakinifu wa Mfuko wa Barabara:**

Imebainika kwamba jumla ya Shilingi Bilioni 6 zilitengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara kwa Unguja na Pemba. Ukaguzi umebaini kwamba

jumla Shilingi Bilioni 3.8 sawa na asilimia 63 ndizo zilizotumika kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo. Jumla ya Shilingi Bilioni 2.2 sawa na asilimia 37 hazikutumika kwa kazi zinazokusudiwa.Kutumika kwa pesa hizo kumepelekea kutokutekelezwa kwa miradi iliyokusudiwa kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kutoa ushauri na miongozo kwa taasisi mbali mbali za Serikali juu ya kuimarisha viwango vya uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu pamoja na uhifadhi na udhibiti wa raslimali umma. Kumekuwa na mafanikio makubwa katika uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu pamoja na udhibiti mzuri wa raslimali za umma kwa Mawizara ya Serikali pamoja na taasisi zake.

Katika kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeendelea kutoa huduma zake za ukaguzi wa mahesabu za Wizara na Serikali pamoja na taasisi ya mashirika yake ikiwemo mahesabu ya Halmashauri za Wilaya katika Mikoa ya Unguja na Pemba.

**Utekelezaji wa Ripoti ya Ukaguzi ya 2012/2013**

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekuwa ikitoa ripoti zenye ushauri na mapendekezo mbali mbali katika usimamizi na matumizi ya raslimali za umma kwa lengo la kuwa na utawala bora unaoheshimu sheria za fedha na ununuzi na sheria nyenginezo.

Kufuatia tathmini ya utekelezaji ya mapendekezo yaliyotolewa tumebaini kwamba mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya ukaguzi ya mwaka uliopita 2012/2013 yamefanyiwa kazi na kuonesha matumaini ya kuimarika kwa nidhamu ya matumizi na raslimali za umma.

**Uwasilishwaji wa Hesabu za Mwisho ya mwaka 2013/2014 kwa Ukaguzi**

Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na mafanikio makubwa katika uwasilishwaji wa hesabu za mwisho ya mwaka kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi. Uwasilishwaji huo umefanywa kwa kuzingatia Sheria ya Fedha Nam.12 ya 2005 Kifungu 24 (2) pamoja na Kifungu cha 8 cha Sheria hiyo ambapo taasisi zote za Serikali zinawajibika kutayarisha na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hesabu za mwaka zinazojumuisha mapato na matumizi ya taasisi husika.

**Mapato na Matumizi:**

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 mapato yaliyokadiriwa kukusanywa ni jumla Shs.429,915,000,331/= hadi kufikia tarehe 30 Juni mapato yaliyokusanywa ni jumla Shs.386,786,000,257/= sawa na asilimia 90 ya makadirio ikiwa ni upungufu wa Shs.43,000,084,000/= sawa na asilimia 10 ya makadirio.

**Mapato Yaliyokusanywa na Mamlaka ya Tanzania (*TRA*)**

Kwa mwaka 2013/2014 makusanyo halisi kutoka kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ambayo yameingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi yalikuwa ni Shs.136,774,000,000/= ambapo inakadiriwa kukusanya jumla ya Shs.147,900,000,000/= ambapo mapato hayo yalikuwa ni sawa na asilimia 92 ya makadirio ikiwa ni upungufu wa 11,179,926,000/= sawa na asilimia 8 ya makadirio.

**Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Zanzibar**

Bodi ya Mapato ya Zanzibar ni taasisi iliyopewa mamlaka na jukumu la kukusanya mapato ya ndani ya kisheria, inawajibika kukusanya mapato mbali mbali kupitia Bodi zilizowekwa na Sheria zilizotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Taarifa ya Ukusanyaji wa Mapato Halisi kipindi cha mwaka 2013/2014 ambayo imeingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yalikuwa ni Shs.156,572,329,000/= ambapo inakaridiwa kukusanya jumla ya Shs.155,300,000,000/=. Hivyo kuonesha ongezeko la mapato ya Shs.1,272,000,327/= sawa na wastani wa moja ya makadirio.

**Ukusanyaji wa Wizara na Taasisi za Serikali**

Kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 taarifa ya ukusanyaji wa mapato ya Mawizara na Serikali na taasisi mbali mbali za Serikali zinaonesha makusanyo halisi ya Shs.14,617,025,025,000/= ukilinganisha na makadirio ya Shs.14,315,331,000/= Hivyo kuonesha ongezeko la makusanyo ya Shs.301,000,764/= sawa na asilimia 2 ya makadirio.

**Mapato Mengineyo**

Kwa mwaka 2013/2014 mapato mengineyo na msaada wa kibajeti wa Kiserikali ilipata jumla ya Shs.57,876,000,759/= ikilinganishwa na makadirio

ya Shs.70,000,000,000/= ambapo ni sawa na asilimia 82 ya makadirio ikiwa ni upungufu wa Shs.12,123,000,241/= ambapo ni sawa na asilimia 17 ya makadirio.

**Hitimisho**

Kwa mara nyengine tena ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufikisha taarifa hii hapa Barazani leo hii. Kwa dhati kabisa Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru wewe mwenyewe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa hatua mbali mbali munazochukua katika kufanikisha lengo la kuimarisha uwajibikaji na utawala bora.

Aidha, ninachukua nafasi hii kuipongeza kwa dhati Kamati ya *PAC* chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa ushauri na maelekezo. (*Makofi*)

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itaendelea na jitihada zake kuongeza viwango vya taaluma kwa wafanyakazi wake, ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya kazi ya ukaguzi yanayotokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi zinazochukuliwa na Baraza la Wawakilishi pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla kusimamia uwajibikaji na uwazi wa matumizi ya fedha ya raslimali umma ili kufikia dhana nzima ya utawala bora.

Ninampongeza *CAG* na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanazofanya. Katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi Ofisi hii inahitaji msukumo mkubwa kutoka Baraza lako Tukufu kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na kuongeza ufanisi katika kazi za ukaguzi na hatimaye kufikia lengo la kuwa na utawala na uwajibikaji katika matumizi ya fedha na raslimali za umma.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana tunakushukuru Mhe. Waziri. Sasa hivi ni nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kuja kutoa ripoti yao.

Mwenyekiti wa Kamati karibu.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* nitatoa nafasi kama muda utaturuhusu zisizozidi tano kwa maswali. Hivyo, naomba wale ambao wanahitaji kuuliza maswali walete majina yao. Ninashukuru.

Mhe. Mwenyekiti karibu!

**Mhe. Rashid Makame Shamsi (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*):** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) juu ya uwasilishaji wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wangu naomba nichukue fursa kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na uwezo wa kutekeleza majukumu yetu kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu. Na mafanikio yake ni kuijenga nchi yetu ya Zanzibar itakayowanufaisha wananchi wetu wa sasa na vizazi vijavyo. (*Makofi*)

Nichukue fursa hii Mhe. Naibu Spika, ya kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wetu adhimu wa Zanzibar kwa kuweza kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kwa asilimia kubwa sana, na hatimaye yeye kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Awamu hii.

Vile vile nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa uteuzi wake, lakini vile vile kwa kuchaguliwa kwa asilimia kubwa na wananchi wake wa Jimbo la Mahonda.(*Makofi*)

Nichukue fursa hii vile vile Mhe.Naibu Spika, ya kuwashukuru Mawaziri wote walioteuliwa na Mhe. Rais kwa kuaminiwa kushika nafasi hizo. Nichukue fursa hii vile vile kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi waliochaguliwa na kuteuliwa na hatimaye kuwepo katika Baraza hili. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sasa niwasilishe shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa lengo la kuzungumza machache na ya umuhimu yanayohusu uwasilishaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa mwaka 2013/2014.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na shukurani hizo, nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri anazoendelea kuzifanya za ukaguzi wa matumizi ya fedha za

umma zinazotumika kwa shughuli mbali mbali za uendeshaji wa Serikali, pamoja na utoaji wa huduma ya jamii licha ya changamoto mbali mbali zinazowakabili kama Ofisi pamoja na wakaguzi wote kwa jumla wao.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imefanya kazi kubwa na nzito ya kufanya ukaguzi katika taasisi mbali mbali za Serikali, kuandaa na hatimaye kuziwasilisha Ripoti hizi nne. Ikiwemo Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*CDF*) kwa kipindi cha mwaka 2011 hadi 2015, na hatimaye Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya *PAC* inaundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 106(g) Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012, na majukumu yake yamefafanuliwa katika Kanuni ya 118(2) kama ifuatavyo:

a) Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya hesabu za mwaka za matumizi ya fedha za Serikali na Mashirika yake na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

b) Kuchambua na kutafakari ripoti yoyote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu pale ambapo Rais aliagiza ukaguzi huo ufanywe.

c) Kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali na asasi zake.

d) Itatoa taarifa yake baada ya kufanya uchunguzi kuhusiana na matumizi ya ziada ya fedha iliyotolewa kwa mwaka wa fedha unaohusika.

e) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

Mhe. Naibu Spika, aidha, katika kufanya kazi zake Kamati ya *PAC* itakuwa na wajibu wa kuchunguza kama fedha zilizooneshwa katika Makadirio ya Matumizi ya Serikali na Mashirika yake zimetumika kama ilivyokubaliwa, matumizi yalikuwa chini ya mamlaka iliyohusika, na kama matumizi yalifanywa kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi hiki, Kamati yetu inaundwa na Wajumbe tisa (9) na Makatibu wawili kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | - | Mwenyekiti. |
| 2. | Mhe. Shaib Said Ali | - | Makamo Mwenyekiti. |
| 3. | Mhe. Abdalla Maulid Diwani | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Rashid Makame Shamsi | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Salma Mussa Bilali | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Shehe Hamad Mattar | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Zulfa Mmaka Omar | - | Mjumbe |
| 10. | Ndg. Nasra Awadh Salmin | - | Katibu |
| 11. | Ndg. Haji Khatib Haji | - | Katibu |

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar, imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na majukumu yake yameelezwa katika kijifungu cha (3) cha kifungu hicho kama haya yafuatayo:

a) Kuhakikisha kwamba, fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria, na iwapo itatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi itaidhinisha fedha hizo zitolewe;

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo, na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya Ukaguzi, madhumuni ya uwasilishwaji wa Ripoti za Mdhibiti katika chombo hichi na madhumuni ya ufuatiliaji na utoaji wa Ripoti kwa Kamati ya *PAC* katika Baraza hili ni kuona kuwa hatimaye dosari za kiutendaji zinazojitokeza zinarekebishwa, na wale wote wanaohusika na ukiukwaji wa taratibu wanachukuliwa hatua. Hii ni kwa maana ya kukomesha vitendo vyote vya wizi, hujuma, uharibifu, ubadhirifu, uzembe na kadhalika katika sekta ya umma.

Mhe. Naibu Spika, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya mwaka 2013/2014 ambayo hivi sasa iko mbele yetu takriban imeendelea kuonesha udhaifu ule ule wa Taasisi za Serikali ambao umekuwa ukibainishwa katika Ripoti kadhaa zilizotangulia.

Mhe. Naibu Spika, Katika Ripoti hii ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali, miongoni mwa dosari zilizobainika katika ukaguzi huo ni kukosekana kwa daftari la kuhifadhi mali za kudumu *(Fixed Asset Register)* katika Mkoa wa Kusini Unguja, kukosekana kwa vitabu vya stakabadhi za ukusanyaji wa mapato katika Baraza la Mji - Wete, malipo yasiyokuwa na vielelezo Tsh. 91,500,000 katika iliyokuwa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na malipo yasiyokuwa na stakabadhi Tsh. 156,402,000 katika iliyokuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Naibu Spika, kuendelea kuwepo kwa dosari hizi katika taasisi za Serikali kunaitia doa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hii ni kwa sababu uwajibikaji, uwazi, uyakinifu na ufanisi katika matumizi ya mali na fedha za umma ni msingi muhimu katika Serikali yoyote inayofuata misingi ya Sheria na Utawala Bora.

Serikali hulazimika kuonesha uaminifu na uadilifu wake kwa walipa kodi kwa kupitia kwa Wawakilishi wa wananchi au kwa wananchi wenyewe moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali, inaonesha kuwa taasisi nyingi zilizokaguliwa zimepata hati inayoridhisha, kwa maana ya kwamba ukaguzi katika taasisi hizo umejiridhisha kutokana na kukidhi viwango vilivyotumika katika uandaaji wa mahesabu, usahihi wa taarifa pamoja na ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi na kupelekea kutoa sura sahihi na halisi ya mahesabu hayo. Miongoni mwa mashirika na taasisi hizo ni Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*), Mamlaka ya Maji (*ZAWA*), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Shirika la Umeme Zanzibar, Shirika la Meli Zanzibar, Shirika la Magazeti ya Serikali,

Shirika la Utangazaji Zanzibar, Chuo cha Uongozi wa Fedha (Chwaka), Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*), Chuo cha Kilimo (Kizimbani), Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar, Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar, Benki ya Watu wa Zanzbar (*PBZ*) na Bodi ya Mapato Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati napenda nichukue fursa hii kuzipongeza taasisi hizo kutokana na matokeo hayo mazuri.

Aidha, tunaziomba taasisi hizo kutobweteka na matokeo hayo na badala yake kuendelea kufuata sheria na taratibu zinazoongoza matumizi ya fedha za umma.

Mhe. Naibu Spika, katika Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*CDF*), kwa kipindi cha mwaka 2011 hadi mwaka 2015 kumebainika dosari mbali mbali zikiwemo, ukiukwaji wa sheria mbali mbali ikiwemo Sheria namba 4 ya mwaka 2012 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Aidha, Sheria ya Fedha namba 12 ya mwaka 2015 na Sheria ya Manunuzi na Ugavi namba 9 ya mwaka 2005, kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, kutoelewana kwa baadhi ya Wajumbe wa Kamati za Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo na Wenyeviti wao, kukosekana kwa kumbukumbu za hesabu pamoja na madaftari mbali mbali yanayohusiana na upokeaji, utoaji na uhifadhi wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya miradi husika.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia kwa kina ripoti hii inaonesha wazi kuwa bado nidhamu ya matumizi ya fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo katika majimbo mbali mbali inakumbwa na changamoto kadhaa. Hivyo, ni jukumu letu Waheshimwa Wajumbe sote wa Baraza hili tukufu kujipanga vizuri zaidi, ili kuhakikisha kuwa fedha katika miradi mbali mbali ya majimbo yetu zinatumika kwa mujibu sheria na taratibu zilizopo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara, si jambo la kutia moyo kuona kuwa katika kila hatua inayohusiana na miradi hiyo kumejitokeza mapungufu mbali mbali. Kwa mfano, katika hatua ya mipango ya awali ya ujenzi wa barabara kasoro za ubunifu, michoro na vigezo kutotayarishwa kwa barabara zilizojengwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na zile zilizojengwa na wakandarasi wa ujenzi wa barabara kabla ya kuingia katika makubaliano ya ujenzi.

Aidha, katika hatua ya taratibu ya manunuzi, iliyokuwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeonekana kutokuweka kumbukumbu zinazohusiana na zabuni katika jalada maalum katika kila mradi.

Katika viwango vya barabara, inaonekana kuwa baadhi ya barabara za Unguja na Pemba ziko chini ya viwango vinavyokubalika kimataifa zikiwemo barabara ya Selem na *Kilwa Roads*. Vile vile, hata katika utekelezaji wa baadhi ya miradi inaonekana kuwa utekelezaji wa miradi hiyo haukufuata masharti yaliyowekwa katika makubaliano.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, kuna haja kubwa kwa viongozi waliopewa dhamana juu ya masuala haya kuweka mkakati maalum utaohakikisha kwamba mapungufu haya yanapatiwa suluhisho la kudumu kwani haikubaliki hata kidogo kuona kwamba Serikali siku zote inatumia fedha nyingi, hasa katika miradi ya ujenzi wa barabara lakini hatimaye utekelezaji wa miradi hiyo unaonekana kuwa na udhaifu mkubwa ambao unaitia hasara Serikali yetu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, matokeo muhimu ya ripoti za ukaguzi ya Afisi hii yana mchango mkubwa katika kujenga Taifa lenye misingi ya Utawala Bora kwa kuwa taasisi za serikali zinapaswa kuwa na shime ya kuchukua hatua za kutatua kasoro mbali mbali zinazobainishwa katika ripoti hizo.

Aidha, Mhe. Naibu Spika, kwa mnasaba huo, viongozi wa taasisi za serikali wana dhima kubwa ya kusimamia vyema utekelezaji wa sheria na kanuni husika, na kuhakikisha kuwa fedha na mali za umma zinatunzwa na kutumiwa kwa uadilifu, ikiwa ni pamoja na kupambana na rushwa.

Aidha, ni vyema kuachana kabisa na tabia ya kuwaacha watendaji wa serikali kukiuka taratibu kwa kisingizio kuwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ipo na itachunguza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa upekee Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa umakini wao wa kunisikiliza wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii, nikitarajia kuwa, wataweza kabisa kutoa michango yao yenye tija juu ya ripoti hizi, kwa manufaa ya nchi yetu na watu wake.

Mhe. Naibu Spika, sasa vile vile nichukue fursa hii adhimu kuweza kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni, kwa kunipa ridhaa yao

ya kunichagua na hatimaye kuweza kunifikisha katika chombo hiki muhimu cha kuwatetea.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, kama nilivyotangulia kusema mwanzo, mna nafasi ya kuuliza maswali. Mpaka sasa hivi nina wajumbe wawili tu ambao wana nia ya kuuliza maswali. Kwa hivyo, kama kuna mwengine atajitokeza basi anakaribishwa. Nitaanza na Mhe. Machano Othman Said.

**Mhe. Machano Othman Said:** Mhe. Naibu Spika, mimi nakushukuru kwa nafasi hii na pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama. Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kuuliza swali moja na ushauri.

Kwanza swali langu ni kwamba katika fedha za *CDF* au Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, nahisi kuna tatizo la kuingiliana kwa kamati pengine ya Mbunge na Mwakilishi, na kwa sababu nia na madhumuni ni kuleta maendeleo kwa pamoja.

Je, isingekuwa vyema kwamba fedha hizi na zile za Mbunge, kukawa na mnyororo fulani wa kuziunganisha ili kile kinachopatikana zile kamati mbili zikakaa kwa pamoja na kuzitumia vizuri. Kwa sababu inawezekana akatumia Mbunge mimi nikaenda kupiga picha na ikawa fedha zimetumika vizuri.

Ushauri wangu Mhe. Naibu Spika, kwa Mhe. Waziri anayehusika na utawala bora, ni kwamba ukiangalia hiki kitabu, mwaka jana tulikuja kukaguliwa wakati mbaya na ndio maana utakuta fedha nyingi unaambiwa hazikutumika, hazijaingizwa maana yake ukaguzi wenyewe ulikuwa mwezi wa 8 na 9, na wakati huo ndio watu wanakwenda mbio na uchaguzi, kwa hivyo majimbo yalikuwa kama hayana wenyewe, lakini bila shaka wajumbe wengi wametumia vizuri fedha hizi.

Mhe. Naibu Spika, ninaloomba kama ushauri wangu, kwa kuwa sasa Baraza limeanza, na kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wengi wameshaunda kamati, na kwa kuwa nyingi ni mpya, kabla ya matumizi itolewe elimu kwa kamati zote za majimbo ili wajue wajibu wao ni nini. Kwa sababu pengine kamati hazijaelewa madhumuni yenyewe, na wananchi wenyewe hawajaelewa hizi fedha ni za nini. Inawezekana zikipatikana fedha hizi mtu anaweza kukwambia nikatie shilingi 500,000/- kwanza nikafanye harusi.

Kwa hivyo, bora tutoe elimu kwa wale wajumbe tisa ikiwezekana na uongozi wa jimbo, halafu tuanze kuzitumia hizi fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jimbo, ni hayo tu Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Machano Othman. Swali la pili litaulizwa na Mhe. Shadya Mohammed Suleiman na baadae atafuata Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mimi nilikuwa napenda kuuliza kwa nini wawakilishi wa viti maalum hawapewi fedha za maendeleo wakati na wao wanachaguliwa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja mpaka matatu.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, naipongeza Ripoti hii ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo wa (*CDF*).

Mhe. Naibu Spika, pia nawapongeza kamati kwa muda mfupi kuweza kufanya kazi yao haraka na kutuletea taarifa hii, hii ndio wakati huu wa hapa kazi tu, unavyotakiwa ufanyike kama hivi.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nashauri, huu mfuko ni muhimu sana kwa wananchi wetu katika majimbo yetu, lakini katika changamoto nilizoona humu kuna baadhi ya majimbo mengi sana katika mfuko huu kwa matumizi yaliyopita umekwenda kivyake vyake, haukwenda kiutaratibu wa kuwatumikia wananchi wetu haukuwasaidia.

Je, hapa kwa hawa walioharibu mfumo mzima wa mfuko huu ni hatua gani zitachukuliwa dhidi yao. Majimbo ni mengi hasa Pemba.

Pili, nimuombe sana Mhe. Waziri kwa kupitia kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Wawakilishi tukapatiwa semina jambo dogo tusilipwe kitu, lakini tueleweshwe madhumuni. Wengine wanaelewa, lakini wengine bado hawaelewi. Kama alivyotangulia kusema Mhe. Machano Othman kwamba, wengine wanasema labda mfuko huu wa Mheshimiwa kwa mipango yake ya binafsi, kumbe kuwatumikia wananchi katika huduma zao za kijamii.

Ombi langu namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tufanyiwe semina fupi ili kuelimishwa, ili wengine wengi wapya tuliokuwemo humu tuuelewe.

Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa fursa na mimi kuuliza maswali mawili tu.

Swali langu la kwanza Mhe. Naibu Spika, nazipongeza zile taasisi zote ambazo zimepata hati katika ukaguzi uliofanyika, lakini kuna taasisi nyingi ambazo hazikupata hati, sasa serikali inachukua hatua gani ili kurejesha nidhamu ya matumizi katika taasisi zetu za serikali.

Mhe. Naibu Spika, kuna eneo jengine tumezoea kwamba wanaosimamia matumizi sana ni ma-*accounting officers*, katibu mkuu pamoja na wahasibu. Lakini utamkuta muhasibu ameharibu katika wizara fulani, muhasibu yule yule anahamishwa na kupelekwa wizara nyengine. Sasa kule alikopelekwa si anaharibu. Kuwe kuna utaratibu ambao wahasibu wanaoharibu kuwekwa *bench* wengine wachukue nafasi. Kuna vijana wengi wana taaluma za uhasibu wachukue zile nafasi.

Kwa hivyo, nilikuwa naishauri serikali kwamba wahasibu wale au ma-*accounting officers* wa wizara wanapoharibu wafanyiwe tathmini, wanapoharibu wasibadilishwe wizara, kule wanakokwenda nako wataharibu na mifano hii imetokezea na ipo.

Kwa hivyo, tukiendelea na mfumo huu lile suala la kufanya kazi kwa mazoea litakuwa linaendelea. Waziri wa Fedha hapa amejikita kwamba atahakikisha katika mwaka huu kutakuwa kuna nidhamu ya fedha kwa upande wa mapato na upande wa matumizi. Kwa hivyo, naiomba serikali hili kidogo lizingatiwe. Hilo lilikuwa swali langu la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, swali langu la pili ni kuhusiana na hii kamati ya maendeleo ya jimbo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wengi wameulizia. Mimi kwa uoni wangu mdogo nimegundua kwamba kuna tatizo moja katika hizi kamati zetu, kwamba hawakupatiwa mafunzo hizi kamati za uendeshaji pamoja na uwekaji wa kumbukumbu vizuri, na ndio maana wakaguzi walipopita walishindwa kupata vielelezo katika ile miradi ambayo imetumika.

Kwa hivyo, naiomba serikali kwamba katika kamati zetu hizi mpya tunazozianzisha hivi sasa, basi wapatiwe mafunzo au semina ili basi ripoti itakayokuja baadae iwe nzuri.

Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Mjumbe, nimepata ombi jengine, kwa hivyo tunaongeza idadi na mamlaka hayo ninayo. Kwa hivyo, sasa hivi nitampisha Mhe. Simai Mohamed Said, na baadae atauliza Mhe. Mwinyihaji Makame.

**Mhe. Simai Mohamed Said:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba bado mimi sio mtaalamu sana. Nilitoka nje niliporudi nimekuta matabu mengi sana, lakini nikaambiwa natakiwa nichangie. Kwa hivyo, nimezunguka hapa nimejua nitajitahidi kile ambacho nahisi kitaweza kusaidia.

La kwanza Mhe. Naibu Spika, kuna utaratibu ambao unatumika na Afisi ya *CAG* ya kukagua mahesabu kwa taasisi ambazo ni za serikali zinazopokea fedha pengine au zinazofanya shughuli ambazo pesa zinakuwa zinapotea. Lakini wanapokwenda kufanya kazi ya ukaguzi ambapo hawa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ili kuweza kukamilisha kazi yao wanakuwa wanatoa kazi ya ziada ili kuwapa yale makampuni kutoka nje, yaani wanatoa tenda ili wapate watu wa ziada zaidi kwenye timu yao ili waweze kukamilisha hiyo kazi na kwenda kuzikagua taasisi mbali mbali za serikali.

Mhe. Naibu Spika, lakini hizi taasisi pia zinatakiwa zilipe fedha kwa ajili ya kuifanya hiyo kazi ya ukaguzi, na kuna mapato pia yanakwenda katika hiyo taasisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Swali langu la kwanza nataka nifahamu, ni kitu gani kinachopelekea hadi hawa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutoa hizi kazi za nje ili kuweza kufanya hiyo kazi ya kukagua hizi taasisi za serikali.

Pili, hizo fedha ambazo wamekuwa wanapokea Afisi ya *CAG* kwa sababu najua ni mabilioni, hizi fedha wamekuwa wanazitumia vipi, hizi fedha ambazo wao wanazitumia kama *retainer*, ni mkato ambao wanazikata hizi kampuni, na ni fedha nyingi, ninapozungumza ni mamilioni au zitakaribia pengine zaidi ya hapo.

Tatu, ni kwa nini hii Afisi ya *CAG*, kwa sababu tayari wao wana mapungufu inawezekana katika hiyo *manpower*, au uwezo wa wafanyakazi wao kukagua hizi taasisi za serikali hawana, lakini wangeweza kutumia pengine njia mbadala

kuwaajiri Wazanzibari wakafanya kazi katika hiyo taasisi, halafu wakatafuta mshauri elekezi kuwasaidia, kuwa-*train* na kuwafundisha, ili kuokoa hayo mapesa yote yanayotumika ambayo inabidi tuzilipe hizi taasisi tofauti.

Sasa hayo ni maswali matatu juu ya hizo fedha.

Pia ningependa kufahamu kwa hiyo miaka ya mbele kutoka hivi sasa tunavyokwenda, ni utaratibu gani sasa wamejipangia, ili kuonana na hizi taasisi za Serikali hazitakiwi kulipa hizi pesa nyingi ambazo zinawatoka hivi sasa, ili kukamilisha hii kazi ya ukaguzi na hatimaye kukamilisha kazi kuja hii ripoti iweze kutoka.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa hii mimi nilikuwa na maswali mawili madogo tu.

Kwanza tunamshukuru sana mkaguzi kwa ripoti yake kupitia Mhe. Waziri nataka kuuliza kwa mwaka wa fedha huu ulioishia tarehe 30 Juni, 2014. Taasisi ngapi za Serikali zimepata hati chafu au isiyoridhisha. Nataka kujua idadi yao, na kama zipo Mhe. Waziri au Serikali ina mipango gani kwa taasisi hizo.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi nami niulize swali moja dogo tu. Kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa ripoti yake nzuri pamoja na watendaji wake.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 85 kuna miradi hapa baadhi ya majimbo pesa zinaonekana, lakini miradi yake mpaka ukaguzi unamaliza kufanyika haujatekelezeka mradi huo.

Swali langu, je, pesa hizi huwa zina utaratibu gani wa kutumika zinarudi Serikali au zinapangiwa vipi.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante kwanza tungelianza na Mhe. Mohammed Aboud ajibu swali linalohusu mfuko wa majimbo, halafu baadae tutampa nafasi Mhe. Waziri wa Sheria, Katiba, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na yeye kujibu masuala yanayofuatia.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nimpongeze sana Mhe.

Waziri kwa kuwasilisha taarifa hii kwa ufasaha mkubwa sana yeye na watendaji wake naamini tumemuelewa vizuri sana.

Aidha nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hii ambaye naye amewasilisha ripoti ya kamati iliyofanya kazi kubwa yenye maelezo ya kina sana, na ambayo maelezo yake Serikali itayafanyia kazi. Kwa hivyo napenda sana kumpongeza Mwenyekiti na kamati nzima kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *CDF* kushirikiana na wenzetu wa upande wa Wabunge. Kwa kuwa tuna sheria mbili tofauti jambo hili litakuwa gumu kidogo, lakini ni vizuri kwa sasa imeonekana wazi kwamba ule mfuko wa jimbo wa Wabunge umefanya kazi vizuri zaidi kuliko mfuko wa Jimbo wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa msingi huo, ni vyema kwa njia moja au nyengine tukaiga ile sheria ya mfuko wa jimbo wa Bunge, kwa sababu ina usimamizi kupitia kwa Halmashauri kitu ambacho kimewezesha miradi ile kufanyika vizuri zaidi, kwa hivyo kuna utaratibu wa kusimamia fedha vizuri zaidi kupitia utaratibu ule kuliko utaratibu wa Sheria yetu.

Kwa hivyo ningelifikiria Wajumbe hapa wangependekeza namna nzuri ya kurekebisha sheria yetu, ili ioane na matakwa ya matumizi ya fedha, kwa sababu kwa sasa inatoa mwanya wakati mwengine kwa baadhi yetu fedha hizi kuzitumia visivyo zikenda nje ya mstari.

Kwa hivyo nadhani jambo zuri, kwa sababu Wizara yetu kwa njia moja au nyengine mwisho wa siku itakuwa dhamana, kwa hivyo itabidi ilete mapendekezo ya namna ya kurekebisha sheria hii ili ioane, na fedha zitumike vizuri kwa manufaa ya wananchi wetu na isiwe kwa watu binafsi.

Ni kweli hususan kwa upande wa Pemba kwa kipindi kilichokwisha hatukuona miradi mizuri kule kwa upande wa Baraza la Wawakilishi, lakini miradi iliyotekelezeka vizuri unaiona kwa upande wa Bunge ambayo kwa njia moja au nyengine ilisimamiwa na Halmashauri.

Kwa hivyo sheria iko wazi, wanaofanya kosa hatua za sheria zitaendelea kuchukuliwa kwa mujibu wa makosa yenyewe, kwa hivyo Waheshimiwa Wawakilishi tulielewe hilo na liwe ni funzo kwa yeyote yule anayekwenda kinyume na utaratibu ajue sheria inambana, hizi fedha ni za Serikali, na lazima zitumike kwa manufaa ya watu wetu kama zilivyopangwa.

Kwa hivyo Waheshimiwa hususan Pemba ambapo makosa yamefanyika zaidi itabidi waitwe wajieleze kwa mujibu wa sheria huko mbele ya safari. (*Makofi*) Kuhusu kwa nini Wawakilishi wa viti maalum hawana mfuko wa jimbo. Hizi fedha za mfuko wa jimbo zinakwenda katika jimbo, zinatumika katika jimbo, kwa hivyo viti maalum labda watoe ushauri ya namna gani ya mfuko wao wanataka, lakini mfuko wa jimbo lazima fedha ziende kwenye jimbo.

Kuhusu semina nafikiri ni wazo zuri ni vizuri tuwe na semina kwa Wajumbe wa Baraza letu na wale watendaji katika mfuko wa jimbo wa kamati zile za maendeleo tuwaalike siku ya semina hiyo, ili mafunzo hayo yaweze kutoa mwanga vizuri tuweze kuelewana tusaidiane. Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Machano Mjumbe wa Kamati anakuja anasema mimi nina harusi yangu anataka umkatie kwenye fedha za mfuko wa jimbo, huo sio utaratibu kabisa, fedha zile ni kwa ajili ya kuongeza nguvu za maendeleo katika maeneo yao, Serikali imeanzisha utaratibu huu ina dhamira kubwa zaidi kadiri itakavyopiga hatua ya kufanya maendeleo makubwa katika mfuko huu na namna ambavyo tutau-*manage* vizuri ndio pale Serikali itaweka fedha zaidi.

Serikali ingependa ijitoe kabisa katika shughuli ambazo zinaleta tija kwa wananchi na ambazo wao wenyewe wananchi wangeona zinafaa katika maeneo yao, kwa hivyo ikasaidia sasa Shughuli za serikali katika kuleta maendeleo kwa wananchi katika maeneo husika. Kwa msingi huo tungependa iwe mfano mzuri ili Serikali ivutike kuongeza fedha hizo. Kwa sababu zitakapoonekana kwamba hazitumiki vizuri, matokeo yake inawezekana kabisa serikali ikaona haupo umuhimu wa mfuko wa jimbo lazima tuambizane wazi, itakapoonekana zinatumika vizuri zinaleta tija kwa wanachi, Serikali itaongeza fedha, itakapoonekana fedha hizi hazitumiki vizuri, hazileti taathira nzuri kwa wananchi wetu, na pia Serikali itaona hakuna umuhimu wa mfuko wa jimbo, kwa hivyo tuwe waangalifu katika matumizi haya.

Kuhusu ucheleweshaji tutajitahidi fedha zifike kwa wakati ili waheshimiwa Wajumbe na kamati zao wapange vizuri ili ziweze kutoa tija iliyokusudiwa.

Kwa wale ambao majimbo yao hawakuomba hizi fedha ama hawakuzichukua fedha, tunajua wako wenzetu walizisusia hizi fedha na hasa niseme wazi ilikuwa ni Mji Mkongwe, naamini mji Mkongwe ule sio Mji Mkongwe wa sasa, Mji Mkongwe wa sasa unachukua fedha kwa ajili ya maendeleo. Kwa sababu Mwakilishi aliyekuwapo ana imani na watu, anajali maendeleo ya watu, anataka kufanya kazi za watu, kwa hivyo atachukua fedha hizi ziende kutumika. Unapewa fedha za Serikali ziende zikatumike kwa maendeleo, yapo matatizo katika Mji Mkongwe kama hukuzitumia maana yake huwapendelei

wananchi wako kupata manufaa ya maendeleo yao, kwa msingi huo fedha inabidi zirudi Serikalini kama hukuzitumia kwa ajili ya maendeleo ya watu.

Mhe. Naibu Spika, kubwa kwenye mfuko wa maendeleo yalikuwa ni hayo. Mimi niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba tutaendelea kushirikiana nao tuhakikishe mfuko wetu huu wa jimbo unafanya vizuri, taratibu za kisheria zinaheshimiwa na maendeleo ya wananchi yanapatikana. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii kwa mara ya pili, lakini kwa dhati kabisa naomba nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kunisaidia karibu kujibu hoja zote na kunibakishia chache tu ambazo na mimi nitajaribu kuzijibu vile vile.

Niwashukuru Wajumbe wote tisa waliochangia na naomba niwataje walioulizia maswali haya.

1) Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa niaba ya Kamati
2) Mhe. Machano Othman Said
3) Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
4) Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
5) Mhe. Yussuf Hassan Iddi
6) Mhe. Simai Mohamed Said
7) Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
8) Mhe. Amina Iddi Mabrouk
9) Mhe. Mohammed Aboud Mohammed

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumzie kidogo masuala mawili hapa wengi tumezungumza kuhusu mfuko wa jimbo yalielezewa huko kwa sababu yanatuhusu katika majimbo yetu.

Vitabu tumekupeni visomeni na mtaona dosari mbali zilizojitokeza katika majimbo yetu, hukufanya wewe lakini limetokea katika jimbo lako. Sasa ni vizuri ukasoma ukaingalia vizuri na baadaye ukajua ni makosa gani yametendeka.

Mimi naunga mkono hoja ya kwamba tuiangalie upya sheria yetu ya mfuko wa Jimbo hakuna matatizo, lakini kuna baadhi ya majimbo yamefanya vizuri sana wametekeleza kwa mujibu wa sheria ile ya mfuko wa jimbo Mwakilishi

mwenyewe ndio anakuwa Mwenyekiti wa ile kamati yenyewe ya jimbo, na Wajumbe wake wanakuwepo pale kwa mujibu wa sheria wako watu tisa.

Sasa kuna maeneo wamekamilisha hizo kamati kuna maeneo mengine Mwenyekiti na watu wake wawili tu na mwenyekiti hafahamiani na msaidizi wake, mwenyekiti anatoa agizo tu tumia twende, haiwezekani pesa ya Serikali ikatumike kienyeji kama hivyo. Kwa hivyo pesa ya Serikali haiwezi kupotea hivi hivi, na kesi ya jinai haiozi hata siku moja, hata baada ya miaka miwili, mitatu, kumi, ishirini inaweza ikafufuliwa tu kama pesa hizi zimetumiwa kwa njia mbaya wahusika watachukuliwa hatua za kufaa.

Serikali inatoa pesa hizi kwa sababu ya kuwasaidia wananchi wetu, sasa haiwezekani wakatokea wajanja wakazitumia wanavyotaka wao wenyewe, tufuateni mifano baadhi ya majimbo wanafanya vizuri na ndio tukaona maendeleo yanapatikana kwa haraka kwa sababu wenyewe wanasimamia vizuri. Sasa wewe mwakilishi umeshakuwa ndio mwenyekiti unatoa maagizo tu haiwezekani, na wewe mwenyewe ufuatilie ukiziachia ndio zitakwenda hizo.

Mhe. Naibu Spika, sasa kuhusu mfuko wa jimbo na mfuko wa Bunge Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameshanisaidia, lakini sheria mbili tofauti hatuwezi kuziunganisha sheria hizi, kila mmoja anajua tukitaka hivyo kama alivyoshauri basi tutizame marekebisho ya sheria zetu tutaona vipi, lakini ile sheria ya mfuko wa jimbo kwa upande wa Mbunge mwenyekiti yupo pale kweli, lakini Halmashauri ndio wanaosimamia.

Kwenye Baraza letu la Wawakilishi mfuko wetu wa Jimbo mwakilishi ndio mwenyekiti tunasimamia wenyewe, kwa hivyo ni sheria mbili tofauti.

Viti vya wanawake na viti maalum, pesa za jimbo hizi jamani, lakini wewe upo jimbo gani, kama upo Chake Chake mwakilishi wako wa Chake Chake anakuhudumia pamoja na wewe, sasa mshirikiane ili muone kwamba mnaweza kufanya vipi.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Wizara ngapi na Taasisi ngapi zimepata hati chafu. Tumekupa vitabu vinne Mheshimiwa visome vizuri utazijua zote hizo tukijaaliwa, lakini *inshaallah* tukijaaliwa ukivisoma na ukiviangalia tutajua Wizara gani sio nyingi sana, *Alhamdullillah* safari hii afadhali mambo yameelekea kuna maendeleo kidogo lakini si nyingi, lakini *inshaallah* tukiangalia kwenye vitabu hivyo tutajua vya kufanya.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi unasema kama hizi taasisi ambazo zimeonekana zina hati chafu wale watendaji waliofanya makosa haya walichukuliwa hatua gani. Mawaziri ndio sisi, watendaji ndio tunao huko Mawizarani, kama nilivyosema ubadhirifu umefanyika kama kumefanyika uhalifu au kumefanyika ufisadi tusiuache, tusimamie, tufuatilie na mule ambamo mlitendeka makosa yale tuchukue hatua za kufaa. Sisi kama ofisi yetu ya *CAG* itaendelea kufuatilia hizi hesabu za 2013/2014, kuna 2014/2015, kutakuwa na 2015/2016, bado tutaendelea kufuatilia huko, kwa hivyo ni kurekebisha hizi kasoro ili zisitokezee tena.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie suala hili la watu ambao hawakuchukua pesa hizi ambazo Mheshimiwa kasema, sasa Mji Mkongwe hawakubahatika pesa zao kuchukuliwa au zikapelekwa kwa maendeleo yao ni dhahiri kama alivyosema waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa huyu hakutaka maendeleo katika jimbo lile, matokeo yake wamekosa zile fursa maalum, lakini *inshaallah* kwa Mwakilishi aliyekuwepo Mji Mkongwe hatusemi fedha zile zitakusanywa zote ambazo hazikutolewa kipindi kile atapewa sasa hivi, aa haiwezekani hivyo. Sasa hivi atangoja kwa mujibu wa bajeti mpya, kwa sababu zile ndio zimesharudi Serikalini zimeshatumiwa kwa maendeleo mengine ya nchi.

Mwisho nichukue nafasi hii Mhe. Naibu Spika, kukushukuru wewe, Waheshimiwa Wajumbe wote, nimshukuru tena *CAG* kwa kazi nzuri na wasaidizi wake, na naomba waendelee kutushauri na kutusaidia katika taasisi zetu.

Kabla sijamaliza maelezo yangu Mhe. Naibu Spika, mimi nimesimama hapa kwa nguvu ya Mwenyezi Mungu lakini pia nawashukuru sana wananchi wangu wa jimbo la Makunduchi, kwa kuendelea kuniamini na naomba waendelee kuniamini na sitowaangusha *inshaallah* wote, na tutaendelea kusaidiana kwa hali na mali kuhakikisha kwamba maendeleo yao yanakwenda vizuri, hata mfuko wa jimbo la Makunduchi umesimamiwa vizuri.

Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Simai Mohamed Said:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona, naona katika majibu aliyotoa Mhe. Waziri mimi sijapata majibu yangu kwenye maswali niliyouliza.

**Mhe. Naibu Spika,** Mheshimiwa Waziri jibu hata kwa kukaa hapo mjibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Unajua ukiwa na watu ambao wanaweka kumbukumbu vizuri unafurahi sana wakati mwengine wanakukumbusha na wewe.

Mheshimiwa hizi taasisi wakati mwengine tunalazimika kuchukua taasisi za nje sio kwa sababu hatuna wataalamu, wataalamu tunao lakini kuna viwango vya utaalamu vinazidiana, ni taasisi zenyewe na mashirika yenyewe yanayosimamia na yanayogharamia, kwa hivyo inabidi wakati mwengine tu-*hire service* kwa wataalamu wa nje ili watusaidie, na kwa kweli wanatusaidia sana.

Mashirika mengine kama aliyoyataja mwenyewe Mhe. Simai Mohamed Said inabidi tuyafanye hivyo, kwa mfano kama *PBZ, ZRB* tunahitajia msaada kutoka kwa wataalamu zaidi kwa sababu yale mahesabu yanakuwa ni pesa nyingi na kiwango ni kikubwa, kwa hivyo inabidi tulazimike, sio lazima wataalamu tunao lakini yale mambo ambayo *CAG* anaweza kufanya kwa taasisi zetu za Serikali hakuna matatizo anafanya mwenyewe, pale ambapo anahitajia msaada ndio Serikali hulazimika kuomba *service* za nje, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kwa leo naona tumemaliza shughuli zetu na baadae kidogo nitamuomba Mwanasheria Mkuu aweze kututengulia kanuni ya muda, lakini kabla ya hapo nimetakiwa kuwakaribisha wageni ambao wamefika hapa, wageni wenyewe ni kutoka Chuo cha Kitaifa cha Mafunzo ya Ulinzi nchini India yaani *Indian National Defence College, New Delhi* wageni hao ni 45 na wamefuatana na wenyeji ambao ni *Nyuki Brigade* wanaongozwa na Admiral Devender Sudan, *you are most welcome, you can sit down now, thank you!*

Waheshimiwa Wajumbe sasa nimpe nafasi Mwanasheria Mkuu anatutengulia Kanuni ya muda kwa ajili ya kuakhirisha kikao.

Waheshimiwa Wajumbe naomba tukubaliane kwamba tulikuwa na ripoti kesho ya *Finance Bill,* ambayo kwa taratibu zetu naomba tuifanye hiyo ripoti kesho kwa sababu muda tunao bado, lakini tutaweza kuisoma kesho.

Samahanini jamani kumbe sijauliza, sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba niulize wale ambao wanakubaliana na ripoti ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora wanyanyue mikono, kwa wale wanaokataa. wanaokubali wameshinda

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nichukue muda huu kumkaribisha Mwanasheria Mkuu atengue kanuni ya muda ili tumalize shughuli yetu ya leo. Mwanasheria Mkuu karibu sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu kwa kuwa shughuli zetu za leo kwa mujibu wa *order paper* tutakuwa tumekamilisha.

Kwa hiyo, naomba Mhe. Naibu Spika, na Baraza lako Tukufu tuweke kando kanuni za 23(4) kwa ajili ya muda wa Baraza ili tuweze kuakhirisha Baraza hadi kesho asubuhi saa tatu barabara.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe naomba kuuliza wale wanaokubali, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba niakhirishe kikao hadi kesho tarehe 26/05/2016 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 5:37 mchana Baraza liliahirishwa hadi*
*tarehe 26/06/2016 saa 3:00 asubuhi)*